Nipashe
Ijumaa Desemba 4, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580419
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**Vijana** wenye kisukari walia na kodi kubwa ya dawa, vifaa tiba

UKURASA 3



**Wataka** kampuni za 'mikopo umiza' kufutiwa leseni

UKURASA 3



**Zidane apewa mechi nne**

UKURASA 20

# Mdee na wenzake bado kukata rufani

• **Ni** kuhusu kuvuliwa uanachama CHADEMA, uongozi wasema... *Endelea ukurasa 2*



MDEE

MBOWE

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### MAREKANI KUENDELEZA USHIRIKIANO SEKTA YA AFYA

MAREKANI imesema itaendelea kushirikiana na Tanzania katika ...

UKURASA WA 19

### UN YASEMA BANGI SIO DAWA HATARI

UMOJA wa Mataifa (UN), imepiga kura kuondoa bangi katika orodha ya kundi...

## Magufuli afuta tena sherehe za Uhuru

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store


## Watano akiwamo baba mzazi mbaroni njama kumuoza binti miaka 14

UKURASA 2



**MICHEZO** SIMBA YAJA NA TIKI-TAKA KWA MKAPA UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

## 400,000 wafanyiwa tohara kujikinga VVU

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

ZAIDI ya vijana 400,000 wenye umri kuanzia miaka 10 na kuendelea na watu wazima mkoani Shinyanga, wamefanyiwa huduma ya Tohara kwa ajili ya kuwakinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

Lengo la mpango huo ambao ulianza mwaka 2011 hadi sasa, pia ni kuwakinga wake zao dhidi ya saratani ya shingo ya uzazi.

Dk. Peter Mllacha, Mratibu wa kudhibiti UKIMWI Mkoa wa Shinyanga, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili, ambapo alisema tohara inamkinga mwanaume kupata maambukizi ya VVU kwa asilimia 60.

Alisema utoaji wa huduma ya tohara kwa wananchi 400,000 katika Halmashauri sita za Mkoa wa Shinyanga, umesababisha kupunguza maambukizi ya VVU toka asilimia 7.4 kwa mwaka 2011/2012 hadi asilimia 5.9 kwa mwaka 2017/2018.

Aidha, Mllacha alisema matarajio yao ni kuwafikia vijana na watu wazima kwa asilimia 90, na mpaka sasa wameshawafikia kwa zaidi ya asilimia 40, na kwamba utafiti waliofanya unaonyesha maambukizi ya VVU mkoani yamepungua kwa asilimia 60.

Pia, alisema kundi la vijana wenye umri wa miaka 10 hadi 20 wamejitokeza zaidi ukilinganisha na kundi la watu wazima na wamekuwa wakitumia njia mbalimbali katika kuwafikia na kuwapatia huduma kupitia katika ofisi za watendaji wa kata na kukarabati vituo vya kutolea huduma.

"Unapofanyiwa tohara unajikinga na maambukizi ya VVU kwa asilimia 60, na unakuwa unamkinga mwenza wako na saratani ya shingo ya mlango wa uzazi, hivyo vijana na watu wazima ambao hawajafanyiwa huduma hii wajitokeza kwenye vituo vilivyopo jirani yao na kupata huduma," alisema Mllacha.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Salama Mbarouk Khatib, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, katika hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Mdee, wenzake bado kukata rufani

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimesema bado hakijapata barua ya kukata rufani kwa wabunge 19 waliovuliwa uanachama kama walivyodai wakati wanazungumza na vyombo vya habari hivi karibuni.

Kimesema kwa mujibu wa Katiba ya chama hicho, bado wana muda wa kufanya hivyo na kinawasubiri.

Wabunge waliofukuzwa uanachama kwa madai ya kuapishwa bila kuidhinishwa na chama ni Halima Mdee, Esther Matiko, Ester Bulaya, Sophia Mwakagenda, Salome Makamba, Naghejwa Kaboyoka, Grace Tendega, Cecilia Pareso, Agnesta Lambart, Nusrati Hanje.

Wengine ni Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Asia Mohammed, Felister Njau, Kunti Majala, Stella Fiao, Anatropia Theonest na Conchesta Rwamlaza.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, alisema kwa mujibu wa Katiba yao, wanatakiwa kukata rufani ndani ya siku 30 tangu kuvuliwa uanachama.

"Mpaka sasa hatujapokea rufani yoyote kutoka kwa waliokuwa wanachama wetu 19 waliofukuzwa, lakini kama katiba yetu inavyosema, bado wana muda wa kufanya hivyo. Kwa hiyo bado wana muda wa kujipanga. Sisi tunawasubiri na tuko tayari kuwasikiliza," alisema Mrema.

Mrema pia alitumia nafasi hiyo kujibu baadhi ya kauli zilizotolewa na wabunge hao 19 katika mkutano wao na waandishi wa habari, ikiwamo ya kushindwa kuitikia wito wa kufika kwenye kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho kwa madai ya kuwapo kwa baadhi ya wajumbe katika kamati hiyo kuhamasisha wanachama kuwafanyia fujo.

Mrema alisema kauli hiyo si ya kweli isipokuwa walitumia kigezo hicho kama kisingizio tu.

"Napenda kutoa ufafanuzi katika baadhi ya hoja kama walivyodai wao kuwa kuna baadhi ya wajumbe wa Kamati Kuu, ambao walikuwa wanahamasisha wanachama ili wawafanyie fujo. Napenda kueleza kwamba chama hakijawahi kuletewa malalamiko yoyote wala ushahidi na waliokuwa wanachama 19 kabla ya kikao hicho juu ya madai hayo," alisema Mrema.

"Walipoandika barua kuhusu hofu ya usalama wao, chama kiliwaelekeza kwamba badala ya kufika makao makuu ya chama kama ilivyokuwa imeelekezwa awali, wafike katika Hotel ya Ledger Plaza Bahari Beach ili wawe huru kufika na kujielekeza mbele ya kikao cha Kamati Kuu," aliongeza na kusisitiza: "Kwa maana hiyo suala hilo limetumika tu kama kisingizio dhidi ya uamuzi wao wa kukwepa kuja kujitetea mbele ya kikao cha Kamati Kuu."

Kuhusu suala la kuomba kuongezewa muda, alisema walifahamishwa kwa barua kuwa wafike mbele ya Kamati Kuu na wawasilishe maombi yao ya kuongezewa muda ili Kamati itafakari hilo.Badala ya kufanya hivyo waliamua kwa makusudi kukaidi kufanya hivyo.

Mrema alisema Kamati Kuu ina mamlaka kwa mujibu wa Kanuni za chama hicho ibara ya 6.5.1(d) kuchukua hatua za dharura bila kufungwa na masharti ya siku 14 isipokua anayelalamikiwa atakua na haki ya kuitwa kwenye kikao.

"Pamoja na nia yao ya kukata rufani, mpaka sasa chama hakijapokea rufani yoyote na izingatiwe uamuzi wa kuwavua nafasi zao za uongozi ndani ya chama na kuwafukuza uanachama utaendelea kutamalaki na unapaswa kuzingatiwa na wanachama wote na mamlaka zote hadi hapo utakapobatilishwa na Baraza Kuu iwapo wahusika wakikata rufani na rufani yao kukubaliwa," alisema Mrema.

# Watano akiwamo baba mbaroni njama kumuoza binti wa miaka 14

**Na Richard Makore,** MWANZA

WATU watano akiwamo baba mzazi wakazi wa Kijiji cha Mwawile, wilayani Misungwi mkoani Mwanza, wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa kula njama za kutaka kumuoza binti wa miaka 14 kwa mahari ya ng'ombe tisa na fedha taslimu Sh. 100.000.

Binti huyo alitaka kuozwa kwa mwanamume mwenye miaka 40, Buholo Lukuyege.

Sakata hilo lilitokea juzi, baada ya muuguzi wa zahanati ya Mwawile kutoa taarifa kwa mamlaka husika kufuatia wachumba hao kufika kwake kwa ajili ya kupima afya zao.

Akizungumzia tukio hilo, mjomba wa binti huyo, Juma Lukuyege, alisema mtoto huyo hakufanikiwa kumaliza elimu ya msingi na aliishia darasa la kwanza.

Alisema baada ya kushindwa kuendelea na masomo, familia ilianza kumuuliza kama anampenda mwanamume aliyetaka kumuoa na yeye alikubali na mipango ya harusi ikaanza. Baba yake mzazi wa binti huyo, Philipo Lutamula, alisema, wakati uchumba huo ukiendelea hadi kulipwa mahari, hakuwapo nyumbani kwake muda mrefu.

Alisema baada ya makubaliano ya kulipa mahari alipigiwa simu na familia yake na yeye akakubali kwa kuwa aliamini mtoto wake amekuwa na anaweza kuolewa.

Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Juma Sweda, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, alikiri watu hao akiwamo baba mzazi kushikiljwa kwa kosa la kutaka kumuoza binti huyo.

Alisema lazima jamii iache kugeuza watoto wa kike mtaji wa kujipatia utajiri wa ng'ombe badala yake wawaache wasome.

Sweda alisema, watu wanaofanya vitendo vya ukatili watashughulikiwa. Alisema atashangaa kuona serikali inashindwa katika kesi hiyo kwa kuwa ushahidi upo wazi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Misungwi, Upendo Naftari, alisema kuna kampeni za muda mrefu za kutokomeza vitendo hivyo vya kikatili. Aliongeza kuwa wataendelea kupambana na vitendo hivyo mpaka vikomeshwe kwa kuwa vinakwamisha ustawi wa watoto wa kike.

Alisema kwa sasa jamii wakiwamo watoto wanavyosikia kampeni mbalimbali za kupinga vitendo hivyo wanaelewa ukubwa wa tatizo na wengine wanatoa taarifa katika vyombo vya dola.

Hivi karibuni wakati wa ufunguzi maadhimisho ya Siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella aliagiza nguvu za kupambana na vitendo hivyo ziongezwe.

Alisema mikoa ya Kanda ya Ziwa ina takwimu za juu kuhusu vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake na kwamba nguvu za ziada zinahitajika kupambana navyo.

Mkuu huyo wa mkoa aliitaka jamii kufichua vitendo vya ukatili wa kijinsia badala ya kuvifumbia macho kwa kuwa vinaathiri maisha ya watu wanaofanyiwa hivyo.

Alimuagiza Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza kusimamia suala hilo ili kulikomesha kwa kuwa vitendo hivyo vinarudisha nyuma maendeleo ya watoto wa kike.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, aliahidi kupambana na vitendo hivyo kama wanavyopambana na majambazi.

"Mkuu wa mkoa agizo lako tutalitekeleza kwa nguvu nyingi bila uoga ili kukomesha ukatili wa kijinsia kwenye jamii," alisema Kamanda Muliro. Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mkuu wa Dawati la Jinsia mkoani Mwanza, Faraja Mkinga, alisema mwaka huu matukio 1,387 yameripotiwa.

Aliongeza kuwa kesi 455 zilifikishwa mahakamani ingawa baadhi ya watu waliofanyiwa ukatili wa kijinsia wanashindwa kutoa ushirikiano kwa kutoa ushahidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Shirika la Kivulini ambalo linatoa msaada kwa watoto wanaofanyiwa ukatili, Yassin Ally, alisema vitendo hivyo bado vinaisumbua jamii.

## HABARI KITAIFA

# Vijana wenye kisukari walia kodi kubwa ya dawa na vifaa

**Na Margaret Malisa**

VIJANA wanaoishi na kisukari aina ya kwanza, wameiomba serikali kupunguza kodi ya dawa za ugonjwa huo zinazoingizwa kutoka nje kwa kuwa matibabu yake ni gharama na familia nyingi hazina uwezo wa kumudu.

Ombi hilo walilitoa jana walipozungumza na Nipashe baada ya matembezi ya hisani yaliyoandaliwa na wanachama wa Lions Club Mzizima, Uhuru na Tanzanite kwa lengo la kuchangisha fedha za kununua bangili maalum kwa ajili ya kuwatambua vijana na watoto wenye ugonjwa huo.

Walisema watoto na vijana wanaoishi na kisukari wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo gharama kubwa za matibabu na jamii kukosa uelewa wa elimu juu ya ugonjwa huo, hivyo wakati mwingine kunyanyapaliwa na kushindwa kuwasaidiwa pindi wanapougua.

Mwenyekiti wa Vijana na Watoto Wanaoishi na Kisukari nchini, George Kwayu, kwa niaba ya wenzake, aliiomba serikali kupunguza kodi za dawa za ugonjwa wa sukari zinazoingizwa nchini hususani dawa za 'Insulin' zinazotumika kwa vijana na watoto kwa sababu zinapatikana kwa gharama kubwa.

"Kwa siku mgonjwa wa sukari anatumia takribani Sh. 50,000 kwa dawa peke yake, bado gharama za upimaji na vijiti maalumu vya kupimia sukari, kitaalamu ni ‚glucose test trips‚‚ mabomba ya dawa ambayo ni kati Sh. 500 na 1,000 kwa maeneo yenye uhaba," alisema Kwayu.

Alisema ni vyema serikali ikawapunguzia kodi wafanyabiashara wanaouza dawa hizo ili nao wapunguze bei na hatimaye zipatikane kwa urahisi na kuokoa maisha ya watoto na vijana wenye tatizo hilo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Umoja huo, Anicet Muchunguzi, alisema wazazi na jamii nzima, hususani shuleni, wanapaswa kutambua ugonjwa huo kwa watoto upo, hivyo waungane na wadau wa afya katika kuwasaidia ikiwa ni pamoja na kuchangia fedha kwa ajili ya kununua bangili hizo maalumu.

Waandaaji wa matembezi hayo na washirika wao, walisema wamekusanya zaidi ya Sh. milioni 10 ambazo zitanunua bangili hizo kwa ajili ya kuwatambulisha watoto na vijana wanaoishi na ugonjwa huo.




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikabidhi cheti cha uanachama wa muda mrefu kwa Mkuu wa Utawala wa Nampak (T) Ltd, Said Rabii, wakati wa sherehe za miaka 60 ya Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na mkutano mkuu wa mwaka, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Dk. Aggrey Mlimuka, Mwenyekiti wa Bodi, Jayne Nyimbo (wa tatu kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Dar, Abubakar Kunenge. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wataka kufutwa kampuni za 'mikopo umiza'

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WALIMU wastaafu wilayani Kahama, wamezitaka mamlaka husika zinazotoa leseni kwa kampuni za ukopeshaji mjini hapa, kuzifuta kwa kuwa zimekuwa zikiwaumiza kwa kuwaongezea riba kubwa wateja.

Kampuni hizo ambazo baadhi zipo kisheria na zingine ni za binafsi, zimekuwa zikiwaumiza watu, hasa walimu wastaafu, ambao wamekuwa wakienda kutafuta msaada wa kupata fedha kwa ajili ya kukidhi maisha yao na wao wamekuwa wakiwaongezea riba kubwa.

Hayo yalisemwa juzi na walimu wastaafu 18 ambao walirudishiwa Sh. milioni 23.6 kutoka kwa wakopeshaji umiza na wadaiwa sugu wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha Walimu Kahama (SACCOS) kutoka kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)) wilayani Kahama.

Mmoja wa walimu hao, Paulina Mlacha, ambaye ni miongoni mwa walimu wastaafu waliorudishiwa fedha zao, alisema kwa sasa walimu wastaafu ambao wanahisi kudhulumiwa na kampuni hizo, ni bora wakatoa taarifa katika taasisi hiyo ili kupata msaada. Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake wakati akikabidhi fedha hizo kwa wahusika, Mkuu wa TAKUKURU wilayani Kahama, Cosmas Shauri, alisema taasisi yake imeokoa fedha hizo kutoka kwa wakopeshaji wawili wa mikopo umiza.

Shauri alisema Sh. milioni 15.4 zimeokolewa kutoka kwa wakopeshaji wa mikopo umiza na Sh. milioni 8.2 zimeokolewa toka kwa wadaiwa sugu wa Walimu SACCOS Kahama.

Aliongeza kuwa fedha zilizookolewa kutoka kwa wakopeshaji umiza, Sh. milioni 9.7 zilitoka Super Salo Investment Limited ya mjini Kahama na Sh. milioni 5.6 ziliokolewa kutoka katika Kampuni ya Ukopeshaji ya Cleophas Credit and Investiment pia ya kahama.

Pia alisema walimu waliokopa kwa wakopeshaji hao walikuwa wakilipa riba kubwa kuanzia asilimia 241 hadi 300 kutokana na mikopo waliyochukua ambayo kwa kiasi kikubwa ilikuwa inawaumiza.

Shauri alisema uchunguzi ulifanywa na taasisi yake ulibaini kuwa Aprili, mwaka jana, Mlacha alikopa Sh. milioni tatu kutoka kampuni ya Cleophace Credit na kutakiwa kirejesha Sh. milionI 12 sawa na roba ya asilimia 300 hadi kufikia Juni, mwaka huu.


**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

**TAARIFA KWA UMMA:**

**USAJILI NA MAOMBI YA LESENI YA BIASHARA ZA UTALII NCHINI KWA MWAKA 2021**

Wizara inaujulisha Umma pamoja na Wafanyabiashara wote wa utalii nchini kuwa, maombi ya usajili na utoaji wa Leseni za Biashara za Utalii (TTBL) kwa Wakala wapya na wanaoendelea kwa mwaka 2021 yameanza kupokewa rasmi. Hatua hii ni kuwezesha upatikanaji kwa wakati leseni za TTBL ambazo hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008. Hivyo, wahusika wote mnahimizwa kuwasilisha maombi ndani ya kipindi tajwa.

Aina za biashara au shughuli za utalii husika ni pamoja na: Tour Operators/Safari Out fitters; Photographic Safaris; Hunting Safaris; Travel Agents; Handling Agents; Overland Tourist Trucks; Hot Air Balloon Safaris; Horse Riding; Tourism Sea Ferries and Boat Safaris; Tourism Water Sports (Big Game Fishing, Scuba Diving etc.); Tourism Recreation (Zoo, Snake Parks etc.); Air Charter Services (Non Schedule Flight); Mountain Climbing or Trekking; Car Rental or Hire; Amusement Centers; Professional Safari Photographers (Filming); Tour Guides; Exclusive Luxury Accommodation Facilities; Lodges; Tented and Mobile Camps; Town Hotels; Vacation Hotels; Villas; Cottages and Serviced Apartments; Motels; Camping and Caravan Sites; Tourism Hostels; Tourism Home Stays; Cultural Heritage Centers; Curio Shops; Cultural Tourism Enterprises na Tour Guides.

Muhimu: Maombi mapya yanapaswa kuambatana na taarifa zifuatazo:- (i) Namba ya Mlipa kodi (ii) Cheti cha usajili wa BRELA au Sole Proprietor Extract/partnership Deed (iii) Uthibitisho wa Uraia

Maombi yote ya usajili na utoaji leseni za biashara za utalii yanafanyika kupitia mfumo wa kielektroniki wa Wizara, MNRT – Portal, unaopatikana katika tovuti ya Wizara www.maliasili.go.tz. Izingatiwe kuwa, ni kosa kisheria kuwasilisha taarifa za uongo na adhabu yake ni pamoja na kufutiwa leseni.

Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu www.maliasili.go.tz au fika kwenye Ofisi zetu za Makao Makuu zilizopo UDOM, Dodoma au Ofisi za Utalii za Kanda zilizopo Jengo la Mpingo, Dar es Salaam; Jengo la PSSSF, Mwanza; Jengo la NSSF, Iringa; na Jengo la TANAPA Makao Makuu, Arusha.

**Imetolewa na:**
**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**S. L. P. 1351**
**40472 DODOMA**

**Simu: +255759907390/+255 684498345/+255 752992644**
**Barua pepe: dt@maliasili.go.tz**
**01 Desemba, 2020**

216027802

Edit with WPS Office

# Pinda awapa mbinu vijana kuhusu ajira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda, amesema tatizo la ajira kwa vijana ni kubwa na kuwataka kuchangamkia fursa zilizopo kwenye kilimo bila kujali elimu waliyonayo.

Pinda aliyasema hayo jana katika mkutano wa mwaka wa kujifunza, ulioandaliwa na Jukwaa la Wadau wa Kilimo Wasio wa Kiserikali (ANSAF) unaofanyika kwa siku mbili jijini hapa.

"Utaona vijana wanazunguka na bahasha wakitafuta ajira. Fursa zimejaa kwenye minyororo ya thamani ya mazao ya kilimo kama ngozi, nyama, maziwa, samaki, kahawa, alizeti, korosho, na mazao mengine. Hakikisheni tu mnazingatia ubora maana ndilo eneo linalosumbua," alisema Pinda.

Alisema zaidi ya vijana 800,000 wanaomaliza shule za msingi, sekondari na vyuo wamekuwa wakienda mijini kutafuta ajira na kuwataka kuondokana na dhana na mitazamo hasi ili kutumia fursa zilizopo kwenye kilimo.

Pinda alisema Tanzania inatumia fedha nyingi kununua bidhaa za ngano na mafuta na kwamba hiyo ni fursa ya kuwasaidia wasomi kuchangamkia kulima mazao hayo.

"Kuna usafirishaji wa chini wa mazao ya bustani ikilinganishwa na Kenya na Ethiopia. Mazao haya yana uwezo wa kutengeneza ajira milioni 2.5.

"Ukichukua dhana kwamba umesoma, ndiyo zinatufanya tusimame barabarani kusema huna ajira wakati fursa zimetuzunguka, Takwimu zilizotolewa na Shirika la Kazi Duniani(ILO) inaonesha Tanzania kuna tatizo la ajira kwa asilimia 11," alisema.

Hata hivyo, aliwataka kutoogopa mikopo bali wahakikishe wanakopa kwa malengo na kupeleka fedha eneo husika ili ziwe na tija.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, alisema serikali ina mkakati wa taifa wa vijana ambao unakusudia kutengeneza mazingira wezeshi kwa vijana ili kuvutiwa katika shughuli za kilimo.

"Tunaandaa mkakati wa pili ambao utaishia juni 2021, ambao lengo ni kumtaka kijana akione kilimo ni biashara, na serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa imekuwa ikitoa mikopo kwa vijana ambayo imesaidia kuimarisha mitaji yao,"alisema.

Kutokana na masharti ya kibenki, alisema vijana wengi wameshindwa kupata mikopo yenye masharti nafuu na kwamba serikali imeagiza taasisi za fedha kutoa mikopo isiyozidi asilimia tisa na kutoa muda wa marejesho ya mkopo.

"Tumekaa na wadau wa benki kuangalia namna ya kutengeneza mazingira nafuu ya kuwafanya vijana kupata mitaji ya kujikita kwenye masuala ya uzalishaji ikiwamo kilimo, mikopo unakuta ina riba asilimia 18 au 19 mazingira kama haya yanawatisha vijana. Pia ukosefu wa masoko na ardhi ni kero zinazowakabili vijana serikali imechukua hatua," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya ANSAF, Edmond Singo, alisema ili kuzalisha ajira za kutosha kwenye kilimo na viwanda kwa vijana, jitihada za makusudi zinahitajika ikiwamo mapinduzi ya uchumi kwa kuongeza ushindani wa kibiashara.

Alisema vijana wanapaswa kupewa elimu stahiki na kuwezeshwa katika fursa mbalimbali.

Singo alibainisha kuwa katika miaka mitano ijayo serikali imepanga kutengeneza ajira milioni nane na kwa maoni ya wengi suala hilo litakuwa gumu kama kilimo na vijana watakosa kipaumbele.

# JPM afuta sherehe za Uhuru

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amefuta maadhimisho ya sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara zilizotarajiwa kufanyika Desemba 9, mwaka huu na kuelekeza fedha zilizokuwa zimetengwa zitumike kununulia vifaa mbalimbali kwa ajili ya Hospitali ya Uhuru.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Rais Magufuli ameagiza Sh. 835,498,700 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya maadhimisho ya 59 ya Uhuru zitumike kwa kazi hiyo.

Majaliwa alitoa taarifa hiyo kwenye sherehe za kuadhimisha miaka 60 ya kuanzishwa kwa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) zilizofanyika katika hoteli ya Serena, jijini Dar es Salaam. Alisema Rais Magufuli ameagiza siku hiyo itumike kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kijamii

Novemba 20, 2018, Rais Dk. Magufuli aliagiza Sh. 995,182,000 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya maadhimisho ya 57 ya Uhuru wa Tanzania Bara, zitumike kujenga Hospitali ya Uhuru, ambayo kwa sasa ujenzi wake umefikia asilimia 92.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya 59 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa mwaka huu inasema; 'Miaka 59 ya Uhuru na Miaka 58 ya Jamhuri: Tanzania yenye Uchumi Imara Itajengwa na Watanzania Wenyewe, Tufanye Kazi kwa Bidii, Uwajibikaji na Uadilifu.'

Waziri Mkuu alisema hadi sasa ujenzi wa hospitali Uhuru umegharimu Sh. bilioni 4.2.

Januari, mwaka jana, wakati akipokea gawio la hisa za kampuni ya Simu ya Airtel, Rais Magufuli aliagiza Sh. 2,415,151,650 zilizotolewa na kampuni hiyo zitumike katika ujenzi wa hospitali hiyo.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kufunga nguzo za taa za barabarani zinazotumia nishati ya jua, katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la kituo cha basi ITV Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Marekani kuendeleza ushirikiano sekta afya

**Na Elizabeth Zaya**

MAREKANI imesema itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kupambana na vifo vya kinamama na watoto.

Balozi wa Marekani nchini, Dk. Donald Wright, alisema lengo ni kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa kuanzia miundombinu yake, rasilimali watu na nyinginezo katika sekta hiyo.

Pia, Dk. Wrigth alisema nchi hizo mbili zitaendelea kushirikiana katika mapambano dhidi ya malaria.

"Watu wa Marekani na Tanzania ni marafiki, hivyo tutaendelea kushirikiana katika kuhakikisha vita dhidi ya malaria na Virusi vya Ukimwi vinafanikiwa kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma za dawa za kufubaza virusi vya Ukimwi (ARV's) kwa wanaoishi na VVU pamoja na kuwakinga akina mama wajawazito na watoto dhidi ya malaria kupitia afua mbali mbali vinafanikiwa,"alisema Wright alipokuwa akizungumza mkoani Arusha wakati wa kutoa elimu ya afya kwa wanawake.

"Mradi wa afya unaojulikana kama 'USAID Tulonge Afya' ni mradi pekee nchini ambao kwa kupitia ufadhili wa serikali ya Marekani umejikita kusaidia mabadiliko ya tabianchi miongoni mwa wanajamii kwa kuhakikisha watu wanachukua tahadhari na kujikinga na magonjwa mbalimbali." Alisema Arusha ni miongoni mwa mikoa 12 inayofaidika na ushirikiano mzuri wa kimaendeleo kati ya Tanzania na Marekani hususani katika masuala ya kiafya kwa kinamama na vijana kupitia mradi wa USAID Tulonge Afya ambao unatekelezwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto na Shirika la FHI360 la Tanzania.

Mwakilishi wa Shirika lisilo ya kiserikali la EMAC, Dennis Kabuta, alisema juhudi zinazofanywa kupitia mradi huo, zinaunga mkono juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa na serikali ya Tanzania katika kupunguza vifo vya akina mama na watoto nchini humo.

Meneja wa USAID Tulonge Afya, Kanda ya Kati na Kaskazini, Japhet Daudi, alisema tangu mwaka jana katika Kanda hizo wamefanikiwa kuwafikia kinamama 682 na kuwapatia elimu ya afya ya uzazi.



Ofisa Mkuu Mkaguzi wa Ndani wa Benki ya NMB, Juma Kimori akizungumza wakati wa mkutano wa mwaka wa wahasibu na wakaguzi wa hesabu unaofanyika Bunju, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yakubali ombi kina Mdee kutambulisha wakili mpya

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana imekubali ombi la wabunge wa viti maalumu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Halima Mdee, Ester Bulaya na Jesca Kishoa, kumtambulisha wakili mpya atakayewatetea katika tuhuma zinazowakabili ikiwamo kufanya mkusanyiko na kutotii amri halali katika Gereza la Segerea.

Kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa maelezo ya awali jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Hata hivyo, kabla kesi hiyo haijaendelea, Mdee, Bulaya na Kishoiya waliiomba mahakama kumtambulisha wakili mpya kwamba kuanzia sasa wakili wao atakuwa, Emmanuel Vkandis.

Pia, washtakiwa wengine wataendelea kuwakilishwa na wakili wa utetezi, Peter Kibatala na Hekima Mwasipu.

Mbali na Mdee, Bulaya na Kishoiya, washtakiwa wengine ni, Boniface Jakobo, Patrick Assenga, Henry Kilewo, Yohana Kaunya, Kedmony Mhembo, Mshewa Karua, Khadija Mwago, Pendo Raphael maarufu kama Mwasomola na mkazi wa Bonyokwa, Cesilia Michael, Happy Abdalla; Stephen Kitomali na Paul Makali.

Hata hivyo, mahakama imeshindwa kuwasomea washtakiwa hao maelezo ya awali na imetoa hati ya kukamatwa kwa washtakiwa wawili, Edgar Adelini, Reginald Masawe, walioshindwa kufika mahakamani hapo bila taarifa yoyote.

Awali, Wakili wa Serikali Ester Martin, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya washtakiwa kusomewa maelezo ya awali, lakini washtakiwa wawili hawajafika na hakuna taarifa yoyote, aliiomba mahakama kutoa hati ya kukamatwa na kupanga tarehe nyingine ya kusikilizwa.

Katika hatua nyingine, mdhamini wa mshtakiwa Kedmony Mhembo, Remigius Bafuluki, amewasilisha ombi la kujiondoa kumdhamini mshtakiwa huyo, lakini hakimu amemwambia atajitoa pale na atapatikana mdhamini mwingine na amemtaka mshtakiwa Mhembo kutafuta mdhamini mwingine.

Mapema mahakamani hapo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Renatus Mkude, alidai kuwa shtaka la kwanza ilidaiwa kuwa Machi 13, mwaka huu katika Gereza la Segerea lililopo Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam washtakiwa wote 14 na wenzao ambao hawapo mahakamani, walikaidi amri halali ya Sajenti John, aliyekuwa na dhamana ya kulinda geti kuu la ngome ya gereza hilo ya kuwataka waondoke.

Mshanga alidai kuwa siku ya tukio la kwanza, washtakiwa wote 14 na wenzao ambao hawapo mahakamani, walifanya mkusanyiko isivyo halali katika ngome ya Gereza la Segerea na kutoa hofu, amani na utulivu kwa majirani.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa siku ya tukio, katika gereza hilo, washtakiwa wote 14 na wengine ambao hawapo mahakamani walishirikiana kufanya uharibifu wa geti kuu la gereza hilo mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania. Shtaka la nne, ilidaiwa kuwa siku ya tukio, Mdee alitamka lugha ya kuudhi ikiwamo kumkashifu Sajenti John wa Jeshi la Magereza huku akimwamuru kufungua geti hilo na kusababisha uvunjifu wa amani.

Shtaka la tano, ilidaiwa kuwa siku na eneo la tukio mshtakiwa Bulaya alitamka maneno ya kuudhi mbele ya Sajenti John wa Jeshi la Magereza, huku akimwamuru kufungua geti hilo na kusababisha uvunjifu wa amani.

Martin alidai katika shtaka la sita, siku na eneo la tukio, mshtakiwa Jacobo alitamka maneno ya kuudhi mbele ya Sajenti John wa Jeshi la Magereza huku akimwamuru kufungua geti hilo na kusababisha uvunjifu wa amani.

# Kihanga arejeshwa kugombea umeya

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (CC-NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) imerudisha jina la aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Morogoro, Paschal Kihanga, kugombea tena nafasi hiyo.

Uamuzi wa Kamati Kuu umechukuliwa baada ya Kihanga na Seif Chomoka kufungana kwa kura baada ya kupigwa mara tatu bila kupatikana mshindi. Ili mshindi apatikane, alitakiwa kupata zaidi ya nusu ya kura za wajumbe.

Jina la Kihanga lililetwa na Naibu Katibu Mkuu wa CCM Tanzania Bara na Mlezi wa CCM Mkoa wa Morogoro, Rodrick Mpogoro. Licha ya waandishi wa habari kutoruhusiwa kuingia ndani ya kikao hicho, Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, alizungumzia namna uamuzi ulivyofikiwa.

"Kama tunavyokumbuka uchaguzi awali ulifanyika lakini mshindi hakupatikana, lakini CCM ina taratibu na kanuni zake zilitumika na Kamati Kuu imeleta jina la Paschal Kihanga kuwa mgombea umeya wa Manispaa ya Morogoro," alisema Shaka.

Baada ya kutoa maelezo hayo, aliwataka madiwani na wagombea kuvunja makundi ya uchaguzi na kufanya kazi kwa ushirikiano kwa nia ya kuleta maendeleo ya Manispaa ya Morogoro.

"Madiwani wamepokea kwa furaha, shangwe na nderemo maamuzi (uamuzi) haya (huu) na wameshaaswa na Mlezi wa Chama Mkoa. Kwa hiyo najua madiwani ni waelewa na wanaelewa taratibu za chama," alisema.

Awali, uchaguzi kumpata mgombea umeya ndani ya CCM ulifanyika Novemba 23, mwaka huu, na Chomoka aliongoza kwa kupata kura 20, akifuatiwa na Kihanga na Mhandisi Hamis Ndwata waliofungana kwa kura 11, hivyo Chomoka akatangazwa mshindi.

Hata hivyo, Kihanga alikata rufani kwa madai mshindi hakupata zaidi ya nusu, licha ya kuwa tayari alishatia saini kukubaliana na matokeo, hivyo CCM Taifa kuamuru uchaguzi wa kumpata mgombea kurudiwa.

Uchaguzi huo ulirudiwa tena kwa mara nyingine na awamu ya kwanza iliyoshirikisha wagombea wote watatu, Chomoka aliongoza kwa kupata kura 21, Kihanga 20, na Ndwata kura moja, hivyo msimamizi wa uchaguzi huo akamwondoa Ndwata na kuwashindanisha Kihanga na Chomoka.

Uchaguzi huo wa marudio kwa mara ya pili, Kihanga na Chomoka walifungana kwa kupata kura 21 kwa kila mmoja na walifungana tena kwa mara ya pili na ya tatu, hivyo kusubiri mapendekezo zaidi ya Kamati Kuu ambayo hatimaye yamerudisha jina la Kihanga.

# Mkalimani akwamisha kesi ya udhalilishaji

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KESI inayomkabili mtuhumiwa, Haroub Abdalla Hamad, (60) mkazi wa Finya Bahrein Wilaya ya Wete, imeahirishwa katika hahakama ya Wilaya ya Wete, kutokana na kutokuwapo mkalimani .

Mkalimani huyo alitarajiwa kumtafsiria mshtakiwa mwenendo wa kesi wakati mashahidi wakitoa maelezo.

Ilidaiwa mahakamani hapo na Mwendesha Mashtaka kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Pemba, Ali Amour Makame, kuwa kesi ilipangwa kusikiliza mashahidi, lakini mkalimani hakutokea.

Alidai kuwa mshtakiwa ni mwenye ulemavu wa kutosikia, hivyo ipo haja ya kuletwa mkalimani ili aweze kuelewa kinachozungumzwa na mashahidi, na kuiomba mahakama kuliahirisha shauri hilo hadi tarehe nyingine kwa ajili ya kusikilizwa mashahidi hao.

"Mheshimiwa hakimu, leo tunao mashahidi wanne, lakini kutokana na hali ya mtuhumiwa kwamba ana tatizo la uziwi, tunaomba kesi hii iahirishwe hadi tarehe nyingine ili aitwe mkalimani", alidai.

Hakimu wa mahakama hiyo, Abdalla Yahya Shamhun, alilikubali ombi la upande wa mashtaka na kusema shauri hilo litarudi tena Disemba 7, mwaka huu kwa ajili ya kusikilizwa mashahidi.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, ilidaiwa kuwa mnamo Oktoba mwaka huu kati ya saa 6:30 mchana na saa 11: 00 jioni, mshtakiwa akiwa katika eneo la Finya Bahrein Wilaya ya Wete, alimfanyia ukatili wa kijinsia mtoto wa kike mwenye miaka mitano bila ridhaa yake.

Hata hivyo ilidai kuwa mshtakiwa alikuwa na lengo la kukidhi matakwa yake ya kingono, hivyo alimfanyia kitendo cha udhalilishaji wa kijinsia kwa kumchezea uume wake katika sehemu zake za siri.

Ilidaiwa kufanya hivyo ni kosa kinyume cha kifungu cha 139 (1), (a), (2), (b), Sheria nambari 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Zanzibar.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TAMISEMI iwaepushe walimu mikopo umiza

**MIKOPO** umiza bado ni kilio kikubwa kwa walimu wengi nchini, ambao kutokana na changamoto mbalimbali za maisha, wamejikuta katika mzigo wa mikopo ambayo baadhi imewachukua maisha yao yote ya kazi wakisumbuka nayo.

Tukio la hivi karibuni ni la wilayani Kahama walimu 19 walikopa Sh. milioni 23.6 ambazo riba yake iliongezeka na kufikia asilimia 300, huku wakidaiwa na Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu.

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wilayani humo iliwasaidia walimu hao ambao walielemewa na madeni, huku mmoja akikopa Sh. 15,410,000 kwa riba ya asilimia 300.

Mmoja wa walimu hao alidai aliingia kwenye mikopo hiyo, baada ya mumewe kupooza na kujikuta hana fedha, na alipoambiwa kuna taasisi inakopesha, alichukua kiasi hicho cha fedha.

Kuna matukio mengi ya walimu ambao wamekopa, kiasi kwamba mwisho wa mwezi hawabakiwi na hats senti moja, kwa kuwa licha ya mikopo rasmi ya kwenye benki mbazo mwajiri ndiye mdhamini, lakini mwalimu huyo huyo amekopa taasisi za fedha, na wengine huenda mbali zaidi wanaacha kadi za benki kwa wakopeshaji ambao mshahara ukiingia tu wanakwenda kutoa.

Baadhi ya walimu maisha yao yamekuwa ya kuhamisha mikopo kutoka kwa mkopaji huyu kwenda kwa mwingine, kiasi cha kushindwa kuwa na utulivu wa maisha na kazi.

Kada ya ualimu imeonekana ni rahisi kuonewa kutokana na uhitaji mkubwa wa mikopo kwa ajili ya kukabiliana na matatizo mbalimbali yaliyopo kwenye maisha yao ya kila siku, au katika kujikwamua kiuchumi.

Kazi ya ualimu inahitaji utulivu wa akili ambao huchangiwa na kuwa na uhakika wa kipato na kutokuwa naa usumbufu, ili kumpika mwanafunzi ambaye atakuja kubobea kwenye fani fulani.

Inapokuwa tofauti, ni wazi kuwa mwalimu hatatimiza wajibu wake ipasavyo, na waathirika wakubwa ni wanafunzi. Ni wazi kuwa mwalimu aliyeelemewa na madeni kiasi cha mshahara wote kwisha, anaishi maisha magumu sana kwa kushindwa kutimiza mahitaji ya msingi kwa familia yake.

Ikiwa mwalimu ataishi maisha haya, na inajulikana hawana semina wala na vyanzo vingine vya kujipatia fedha nje ya mshahara, maana yake atashindwa kutimiza wajibu wake ipasavyo.

Wakopaji hao wanaendelea kuwaandama walimu hao kiasi cha kusubiri mafao yao ili kupata fedha. Kipindi mwalimu anasubiri mafao yake, anakuwa ameingia kwenye mikopo.

Tunafikiri ni muhimu sana kwa TAMISEMI kuingilia kati kwa kuweka utaratibu wa walimu kukopa, maana kinachoonekana walojitokeza kulalamika ni wachache kati ya wengi, walioumizwa.

Tunaamini ukiwapo utaratibu huo pamoja na kuwazuia kukopa kwenye taasisi n zisizo rasmi, itasaidia sana kuwaepusha walimu kuishi maisha ya msongo wa mawazo kwa kukosa kipato pamoja na itaepusha taasisi zinazoanzishwa kuwatega walimu wanapopata kipato.

Ni vyema Maofisa Elimu Sekondari na Msingi wakafuatilia suala hili kwa kushirikiana na Chama Cha Walimu Tanzania (CWT), ili kuwaokoa walimu katika madhila magumu wanayolazimika kupitia.

Tunaipongeza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kwa kazi nzuri ya kuwasaidia wanaodhulumiwa haki yao kutokana ni mikataba laghai ambayo huwagharimu kwa maisha yao yote.

Bado kuna wakopeshaji wa riba kubwa wa taasisi na watu binafsi ambao hufanya kama biashara na wateja wao wakubwa ni walimu, ni lazima kufuatilia kwa karibu na kuchukua hatua ili kukomesha tabia hiyo.

Inajulikana wazi kuwa riba za mabenki zinawekewa viwango kwa maelekezo ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ambayo ni msimamizi wa benki. Ni lazima taasisi hizi zikaacha ulaghai kwa kutumia shida za walimu kuwadhulumu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kwa hiki kilio cha VVU na vijana, naungana na karipio la Majaliwa



Na Yasmine Protace

**KUNA** watu wasio na huruma kwa watoto wadogo wa kike. Hawana ama fursa au hata chumba cha staha na huruma kwao.

Wanaamua kufanya nao mapenzi wakati wakijua ni ukatili na usemi wa Mama Salma Kikwete "mtoto wa mwenzio ni wako' haiwahusu, wao 'mafataki' wako kiguu na njia waking'ang'ania la 'mtoto wa mwenzio mkubwa mwenzako.'

Ni mengi tu yameshafanyiwa kazi, hebu tutafakari ya hukumu za miaka 30 maisha, kutoka ile sheria ambayo ni moja kwa moja, iko kumlinda mtoto na binti kwa nafasi ya pekee.

Hapana shaka, sote tunaona na kusikia, kinachowakuta watoto wetu wanaokatiza masomo huko waliko, kikubwa ni simulizi za mimba.

Serikali haichoki ikisonga vitani na askari walio na silaha begani au kifuani, wenyewe wanaita 'haipoti.' Eti na mafataki baadhi yao nao hivyo hivyo... mtashindana na serikali nyie, pia wenye serikali yao na watoto wao yenye hasira nanyi, mtaweza? ... inahusu!

Niwape mchapo! Hivi karibuni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwanyooshea kidole cha ukali wanaofanya mapenzi na mabinti, hali inayosababisha kuwaharibia malengo yao ya baadae. Majaliwa alitoa kauli hiyo alipohutubia kwenye Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, katika uwanja wa Mandela mjini Moshi, mkoa Kilimanjaro, ikibena kaulimbiu "Mshikamano wa kimataifa, tujumuike pamoja".

"Nataka niwakumbushe na kutoa tahadhari kwa wale watu wazima mnaofanya mapenzi na vijana wadogo wa kike, ole wenu, ole wenu, ole wenu!" aling'aka Waziri Mkuu katika ishara ya kutokubaliana na hilo hata kidogo.

Anasema, takwimu za maambukizi mapya ya VVU zinaonyesha kuwapo asilimia 40 ya maambukizi kwa vijana na kati yao asilimia 80 ni mabinti, huku akiweka wazi vijana ni kundi linalokabiliwa na changamoto kubwa ya maambukizi mapya ya VVU nchini.

Majaliwa, anaendelea kusema kundi la vijana na hasa wa kike lipo hatarini kupata maambukizi mapya na uchambuzi wa kimazingira unaonyesha kuwa sababu za vijana kuwa hatarini kuambukizwa VVU, inajumuisha kuanza ngono katika umri mdogo.

Katika hili, Waziri Mkuu ambaye kitaaluma ni mwalimu, anasema vijana wadogo wa kike kuwa na uhusiano wa kingono na wanaume wenye umri mkubwa na hakuna matumizi sahihi na endelevu ya mipira ya kike na kiume.

Wito wake Majaliwa ni kwamba, vijana waanze kujitambua na kuthamini maisha yao kwa njia ya kujikinga na maambukizi mapya ya VVU, huku akiwakumbusha kwamba wao ndio nguvu kazi ya Taifa. Kwa wale wanaoishi na virusi, rai yake kubwa ni kwamba wasiache kutumia dawa za ARV, wakiwa wafuasi sahihi wa maelekezo ya matabibu katika kufubaza VVU na kuimarisha afya zao.

"Natoa wito kwa vijana kujitambua na kuthamini maisha yao, kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU kwa kuwa ninyi ni nguvu kazi na Taifa linawategemea. Wale wanaoishi na VVU, waendelee kutumia dawa za ARV kwa ufuasi sahihi bila ya kuacha, ili kuvifubaza VVU na kuimarisha afya zao,"anasema.

Hapo, pia Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Profesa Mabula Mchembe, anaendeleza hoja kuwa Tanzania na dunia kwa ujumla, zimepiga hatua kubwa katika jitihada za kukabiliana na janga la VVU na UKIMWI,

Anasema wakati nchi inaelekea kufikia malengo ya 93, vikwazo na vipaumbele vimeendelea kubadilika, kutokana na mafanikio ya mwitikio wa mapambano.

Takwimu zinaonyesha wanaume, watoto, vijana wanaopevuka na wadogo ndio wako katika tabia hatarishi, na wavivu kutambua hali zao, wakiwa na ufuasi hafifu wa tiba na ufubazaji wa VVU usioridhisha.

Hata hivyo, Prof. Mabula Mchembe, anasema serikali inaendelea na jukumu la kutafiti, kuandika na kusambaza taarifa za kitaalamu zinazochambua na kutoa suluhisho la magumu yanayohusu sera, miongozo na taratibu za huduma na afya ya VVU na UKIMWI.

"Tunalo jukumu sasa la kutafiti, kuandika na kusambaza taarifa za kitaalamu zinazochambua na kutoa suluhisho la changamoto hizi, ili sasa yatumike kuhuisha sera, miongozo na taratibu za huduma na afua za VVU na UKIMWI", anahitimisha.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi Kilele cha Kilimo cha Maua, Mboga, Matunda na Viungo (TAHA), Jacqueline Mkindi (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kongamano la kikanda lenye lengo la kuongeza hamasa katika kuwekeza na kuibua fursa za biashara katika mazao ya bustani nchini litakalofanyika kesho. Kushoto ni Mkurugenzi wa uhamasishaji na uwekezaji Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), John Mnali na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Maendeleo ya Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), Geoffrey Kirenga.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge ataja mwarobaini uhaba madawati Mkuranga

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

MBUNGE wa Mkuranga, Abdallah Ulega, amesema katika kipindi chake cha miaka mitano, atahakikisha karakana ndogo ndogo zinaanzishwa vijijini ili kurahisisha utengenezaji wa madawati.

Ulega aliyasema hayo juzi mjini hapa wakati wa uzinduzi wa karakana iliyoanzishwa na Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filberto Sanga, kwa ajili ya kutengeneza madawati kwa gharama nafuu.

Alisema uanzishwaji wa karakana hizo utasaidia kumaliza kero ya madawati katika shule za msingi na sekondari katika jimbo la Mkuranga.

"Tayari nimeandaa andiko langu na wadau nitalifikiksha kwa Mkuu wa Mkoa akilipitisha mpango wetu utafanikiwa na tutaanzisha karakana katika maeneo mengi ya jimbo letu na tutaondoa kero ya uhaba wa madawati," alisema Ulega.

Pia alisema kupitia karakana hizo, vijana wanaohitimu elimu ya msingi na sekondari katika maeneo hayo, watapata fursa ya kujifunza ufundi seremala na kujiajiri badala ya kukaa vijiweni.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, alizindua karakana iliyoanzishwa na Sanga, lengo likiwa ni kurahisisha utengengenezaji wa madawati, viti na meza kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Ndikilo alimpongeza mkuu huyo wa wilaya kwa ubunifu huo ambao alisema utaharakisha shughuli ya utengenezaji wa madawati kwa haraka.

Sanga alisema madawati yanayotengenezwa katika karakana hiyo iliyoko ofisini kwake, yatakuwa yanauzwa kwa Sh. 50,000 tofauti na yanayouzwa nje ya karakana kwa Sh. 150,000 kila moja.

Katika uzinduzi wa karakana hiyo, ilifanyika harambee na zaidi ya Sh. milioni 26 zilipatikana ambazo ni fedha taslimu na ahadi, huku Ulega akichangia Sh. milioni 2.2.

# Watalaam wakumbushwa matumizi mtandao

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WATAALAM kutoka taasisi mbalimbali nchini wamekumbushwa matumizi ya rasilimali za mtandao kwa ajili kufanya utafiti na ufundishaji.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini Mwanza na Katibu Mkuu wa Shirikisho la Maktaba za Vyuo Vikuu na Vyuo vya Utafiti (COTUL), katika mkutano wa mwaka wa wakutubi na watafiti.

Alisema machapisho pepe ya kusoma kwa mitandao yanamfanya mtu kwenda na wakati na kupata taarifa sahihi za wakati uliopo.

Alihimiza taasisi ambazo hazijajiunga katika mfumo huo kufanya jitahada zijiunge na kununua machapisho kwa gharama nafuu.

Dk. Msonge alisema siku za nyuma machapisho hayo yalifadhiliwa na taasisi za nje, lakini baada ya kujitoa taasisi mbalimbali zimeungana ili kuendelea kupata maandiko hayo yenye tija na yanayoweza kukuza uelewa wa mtu.

"Machapisho hayo ya online tukiungania na kulipia kwa pamoja gharama ni nafuu ambapo taasisi moja inachangia shilingi kati ya milioni tatu hadi 10 kulingana na ukubwa wa taasisi yenyewe," alisema Dk. Msonge. Alisema watashirikiana na serikali ili waweze kununua machapisho mengi kwa kuwa uchangiaji wa fedha kutoka kwa taasisi wanachama pekee hautoshi kuyanunua.

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma cha Mtakatifu Agustino (SAUT), Pontien Ndabaneze, akizungumzia utalaam huo, alisema taasisi nyingi hazitumii vyanzo vya habari vinavyo ratibiwa na COTUL.

Alisema maarifa yanayopatikana kwa usomaji wa maandiko kupitia mtandao ni muhimu kwa wadau zikiwamo taasisi za elimu na tafiti.

Mkufunzi Msaidizi wa Ukutubi kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Lucy Kasuke, alisema kupitia mtandao wanaweza kufanya utafiti wenye tija.

# SADC yatajwa kuwa fursa soko mazao ya bustani

**Na Beatrice Moses**

UWAPO wa Kanda za Kibiashara za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) zinazokadiriwa kuwa na idadi ya watu milioni 500, inatajwa kuashiria fursa kubwa ya soko la bidhaa za mazao ya bustani.

Hayo yalibainishwa jana na Mtendaji Mkuu asasi ya mazao ya bustani (TAHA), Dt. Jacqueline Mkindi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, kuhusu kuungana na Wizara ya Kilimo kuandaa kongamano kubwa la uwekezaji la kikanda linalolenga kuongeza hamasa kwenye uwekezaji wa mazao ya bustani ambayo ni mboga na matunda.

Dk. Mkindi alisema kongamano jilo linastarajiwa kufunguliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kesho jijini Dar es Salaam. Alisema hatua ya TAHA kuungana na Wizara ya Kilimo kufanya kongamano hilo ni uamuzi wa utekelezaji wa maagizo ya Rais John Magufuli wa kuhakikisha uwekezaji na upatikaji wa masoko ya bidhaa na huduma katika tasnia ya kilimo cha mazao ya bustani zinaongezeka.

"Ili kuhakikisha sekta ya kilimo cha mazao ya bustani inaendelea kukua kwa kasi kwa ushirikiano wa Serikali na sekta binafsi katika kutekeleza vipaumbele vilivyotajwa na Rais Magufuli katika hotuba yake ya Novemba 13, mwaka huu, kuna maeneo ambayo yanatakiwa kuwekeza nguvu ni pamoja na kufanyika utafiti wa kutosha wa masoko na mbegu bora," alisema Dk. Mkindi

Alisema hiyo ni fursa kubwa kwa wadau wa sekta binafsi kwa kushirikiana na serikali kuwekeza katika mnyororo wa thamani wa tasnia ya kilimo cha bustani,kutafungua fursa za kibiashara za ndani na kati ya nchi na nchi, kuleta uhusiano linganifu wa kibiashara utakaonufaisha pande zote pamoja na kubadilishana taarifa.

"Kupitia kongamano hili washiriki watapata nafasi ya kutambua fursa mbalimbali za uwekezaji na masoko ya bidhaa za mazao ya bustani katika masoko ya kikanda na Kimataifa, pia litatoa fursa kujadili changamoto mabalimbali za biashara za kimataifa na jinsi ya kuboresha na kuinua viwango vya mazao ya bustani ili kukidhi mahitaji ya kimataifa," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha SAGCOT, Geoffrey Kirenga, aliwasihi wanahabari kuhakikisha wanawezesha taarifa za uwekezaji huo kuwafikia wananchi, wazipe kipaumbele habari hizo ili kuhamasisha uwekezaji ambao hatimaye utasaidia jamii kujikwamua kiuchumi.

Alisema vyombo vya habari vikiripoti jinsi ambavyo watu wanaweza kupata fedha za mitaji za kuwekeza kwenye miradi hiyo, pia mahali ambapo masoko inapatikana ni hatua mojawapo muhimu itakayosaidia katika kuinua sekta hiyo na kusaidia kuleta mafanikio.

Mkurugenzi wa Uhamasishaji na Uwekezaji kutoka Kituo cha Ewekezaji (TIC) John Mnali, alisema serikali inaendelea na juhudi za kuhakikisha uwekezaji katika kila sekta unakuwa na manufaa ikiwa ni pamoja na kuondoa vikwazo ambavyo vimekuwa vikizua malalamiko.

# NBC yatoa saruji mifuko 236 kuboresha elimu Dar

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa mifuko 236 ya saruji kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi 13 katika Manispaa ya Temeke ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wake katika kuboresha ustawi wa elimu katika manispaa hiyo.

Mifuko hiyo ilikabidhiwa kwa Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Deogratius Lukomanya na Mkuu wa Huduma za Wateja wakubwa wa benki hiyo, Linley Kapya, ambaye pia aliahidi kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu, afya, mazingira na maendeleo ya jamii.

Kapya alisema benki hiyo ina utamaduni wa kurejesha kwa jamii sehemu ya faida inayopatikana kutokana na shughuli zake za kibiashara na mchango huo ni sehemu ya mkakati wa uwajibikaji wa kijamii wa benki hiyo.

Aliongeza saruji hiyo itasaidia kuboresha ubora wa elimu kwa kuwa zitasaidia katika kuboresha shule ambazo hazijakamilika, hivyo kuhakikisha mazingira mazuri ya ufundishaji kwa walimu na wanafunzi.

"Leo tunagawana faida yetu na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa lengo la kuboresha miundombinu ya shule katika manispaa hii. Kama taasisi ya kifedha inayofanya kazi pia katika eneo hili, tuliona kuwa ni muhimu kuunga mkono mpango huu ili turudishe sehemu ya faida tunayopata kwa jamii, " alisema.

Alidokeza kuwa msaada huo ulitolewa baada ya maofisa kutoka Manispaa hiyo kuiomba benki msaada wa kukarabati na kujenga shule za umma zilizozunguka katika manispaa ambazo zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ukiwamo uchakavu na ubovu wa miundombinu.Lukomanya, aliishukuru NBC kwa msaada huo. Alielekeza shukrani zake kwa benki hiyo akisema shule nyingi katika manispaa hiyo kwa sasa zinapitia marekebisho na ujenzi wa miundombinu yake, hivyo msaada huo utasaidia kukamilisha miradi hiyo.

Alizitaja shule zitakazonufaika ni Shule za msingi Toangoma (20), Charambe (15), Faraja (10), Mbagala (20), Marten Lumbanga (10), Kibonde Maji (20), Kilimahewa (15), Kingugi (15), Ukombozi (20), Likwati (15), Yombo Dovya (20), Kizuiyani (36) na Nzasa (20).

Lukomanya alitoa wito kwa taasisi zote za kifedha katika wilaya hiyo kuunga mkono jitihada hizo ili kusaidia sekta ya elimu kwa kuwa zimekuwa zikinufaika na walengwa wa misaada hiyo wakiwamo walimu.



Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Deogratius Lukomanya (kushoto), akipokea msaada wa mifuko ya saruji 236 kutoka kwa Mkuu wa Huduma za Wateja wakubwa wa benki ya NBC, Linley Kapya, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi 13 katika Manispaa hiyo, ikiwa ni mwendelezo wa mkakati wa benki hiyo katika kuboresha ustawi wa elimu nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji Mkuu apewa tuzo ya haki kwa makundi maalum

**Na Mary Gwera**

CHAMA cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kimempatia tuzo ya pongezi Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Hamis Juma, kutokana na jitihada zake za kuhakikisha wanawake na watoto wenye uhitaji maalum wanapata haki.

Akikabidhi tuzo hiyo maalum ofisini kwa Jaji Mkuu jana, Mwenyekiti wa TAWLA, Lulu Ng'anakilala, alisema kuwa chama hicho kinatambua na kupongeza jitihada za Prof. Juma kwa kuhakikisha haki ya kinamama na watoto zinapatikana.

Pia alisema tuzo hiyo ni kwa ajili ya kumpongeza kwa jitihada za kuhakikisha mashauri ya mirathi yanaondoshwa kwa wakati.

"Tunashukuru kwa kuendelea kutuunga mkono katika kuhakikisha haki za wanawake na watoto zinapewa umuhimu wake. Katika hili tunatambua jitihada zako za dhati, hivyo tumeona ni vyema tukukabidhi tuzo hii maalum ili kutambua mchango wako," Ng'anakilala alimweleza Jaji Mkuu.

Prof. Juma alishukuru kwa tuzo hiyo na kuwahakikishia wanachama wa TAWLA kuwa ataendelea kutoa ushirikiano katika kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati.

Pia aliwataka wanachama hao kushiriki na Mahakama katika kuwaeleza wananchi kuhusu taarifa mbalimbali za Mahakama ikiwamo maboresho yaliyofanyika na yanayoendelea kufanyika katika kuhakikisha huduma ya utoaji haki inapatikana kwa wakati.

Jaji Mkuu alitumia fursa hiyo kutoa rai kwa wananchi kuhakikisha wanapata taarifa sahihi za Mahakama kwa kutembelea vyanzo vya habari vya kiofisi ikiwamo tovuti ya Mahakama ambayo ni www.judiciary.go.tz.

"Ili kupata taarifa sahihi za Mahakama, endapo taarifa husika haipo kwenye gazeti au chombo kingine cha habari, ni vyema kutembelea vyanzo rasmi vya habari zetu ikiwamo tovuti ya Mahakama. Kupitia vyanzo hivyo, mtu anaweza kupata taarifa muhimu ikiwamo kujua kesi yake imefikia wapi na kadhalika," alisisitiza.

# Mahakamani tuhuma za kusafirisha heroin

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Mwalimu Juma, amefikishwa mahakamani akikabiliwa na tuhuma za kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin zenye uzito wa kilo 3.14.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Yusto Ruboroga.

Wakili wa Serikali, Neema Mushi, alidai kuwa, Oktoba 17, mwaka huu, eneo la Azam Malinyi, wilayani Ilala jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alikamatwa akisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin.

Kabla ya kusomewa mashtaka hayo, Hakimu Ruboroga alimwambia mshtakiwa haruhusiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Mtuhumiwa alirudishwa rumande na kesi ilihahirishwa mpaka Desemba 8, mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Waandishi wahimizwa kushiriki Tuzo za EJAT

**Na Paul Mallimbo**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) kwa kushirikiana na washirika wake linawahimiza waandishi wa habari kuendelea kushiriki katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2020 kwa kuandika habari zenye kukidhi vigezo vya mashindano hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, alizindua EJAT 2020 Septemba 28, 2020, mkoani mwake katika kilele cha Tuzo za mwaka 2019.

Akizungumza katika Tuzo za 2019, alisema waandishi wa habari wanafanya kazi kubwa ya kuielimisha jamii na kwamba kama isingekuwa vyombo vya habari jamii isingekuwa na taarifa kuhusu ugonjwa wa Covid-19 ambao ulisababisha shughuli za kiuchumi kusimama.

Hii ni kwa mara ya 12 kwa Kamati ya Maandalizi ya EJAT kuandaa mashindano hayo ambayo kwa mara ya kwanza yalifanyika mwaka 2009.

Tuzo hizo zinalenga kuwatambua na kuwatuza waandishi wa habari waliofanya kazi zao vizuri katika makundi mbalimbali ya kushindaniwa.

Washirika wa EJAT 2019 ni pamoja na Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika- Tawi la Tanzania (MISA-TAN), Wakfu wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) na Chama Cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

Wengine ni Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), HakiElimu, Sikika na Agriculture Non-State Actors Forum (ANSAF).

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, alisema kwa uzinduzi huo waandishi wa habari wa magazeti, radio, habari za mtandao (online) na runinga wanakaribishwa kuanza kuwasilisha kazi zao kwenye Baraza katika makundi ya Tuzo za Uandishi wa Habari za Uchumi na biashara na Fedha na Tuzo ya Uandishi wa Habari za Michezo na Utamaduni.

Makundi mengine kuwa ni Tuzo ya Habari za Biashara ya Kilimo, Elimu, Utalii na Uhifadhi, Uchunguzi, Data na Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Pia, Mpiga Picha Bora - Magazeti, Mpiga Picha Bora - Runinga, Mchora Katuni Bora, Tuzo ya Uandishi wa Habari za Jinsia na Watoto, Habari za Gesi, Mafuta na Uchimbaji Madini na Habari za wenye Ulemavu.

Kajubi alisema Tuzo hizo zitakuwa na makundi ya Uandishi wa Habari za Afya, Habari za Ubunifu na Maendeleo, Usalama Barabarani, Habari za Hedhi Salama na Kundi la Wazi.

Aliwakumbusha waandishi wa habari kuwa fomu za ushiriki wa EJAT 2020 zinapatika katika tovuti ya Baraza la Habari Tanzania www.mct.or.tz, na mwisho wa kuwasilisha kazi kwa ajili ya mashindano ni Januari 31, 2021.

Baadhi ya vigezo vinavyotumika katika tuzo hizo ni pamoja na mwandishi kuwasilisha kazi ambayo imesaidia kutoa maarifa mapya kuhusu masuala muhimu katika jamii.

Habari iwe na upekee, umahiri katika matumizi ya lugha, ionyeshe ujasiri katika kuitafuta na kuiandika, iwe imezingatia maadili na weledi wa taaluma ikiwa ni pamoja na kuandika ukweli, usahihi wa taarifa na urari wa vianzo vya habari.



Mwalimu Vivian Ugulumu, akichangia hoja wakati wa semina kuhusu siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Balozi wa Ireland aguswa matukio ukatili wa kijinsia

**Na Christina Mwakangale**

BALOZI wa Ireland nchini, Adrian Fitzgerald, amesema kuna ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia (GBV) duniani, hususan ukatili wa majumbani, na kwamba matukio machache hutolewa taarifa.

Amesema takwimu za Umoja wa Mataifa (UN) zinaonyesha wasichana na wanawake milioni 243 walitendewa ukatili na ndugu, marafiki au majirani.

Balozi Fitzgerald aliyasema hayo kwenye mjadala kuhusu kumaliza ukatili maeneo ya kazi, uliokutanisha asasi, taasisi na vyama vya wafanyakazi jijini Dar es Salaam, ilioandaliwa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF).

Alisema katika siku 16 za kupinga ukatili duniani, pamoja na jitihada za wadau kutoa elimu kwa jamii kuondokana na matukio hayo ukatili uliongezeka zaidi kipindi cha ugonjwa wa corona.

"Takwimu za Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), inaonyesha Tanzania, asilimia tisa ya waliotendewa ukatili ndio pekee walitafuta usaidizi wa kisheria, polisi, wahudumu wa afya, matukio mengine yanayotokea hayaripotiwi," alisema Balozi Fitzgerald.

Kipindi cha Corona wasichaba waliingia katika ndoa na mimba za ututoni kwa kukazimishwa. Tutoe taarifa za matukio haya kuondokana na GBV," alisema balozi.

Aidha, aliipongeza serikali ya Tanzania kwa kuchukua hatu za kukabiliana na matukio hayo, ikiwamo kuanzisha madawati ya kijinsia.

Afisa Ustawi wa Jamii Mwandamizi kutokaWizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Darius Damas, alisema tayari kuna madawati 420 vituo vya Polisi na Jeshi la Magereza madawati 161, ili kulinda haki za wanawake na watoto. "Tuna maeneo au mahabusu maalum ambayo ni kwa ajili ya watoto ambao wanakumbana na ukiukwaji wa Sheria Dar es Salaam tuna mahabusu ya watoto Upanga na Maadilisho Irambo, Mbeya," alisema Damas.

# Madiwani Nachingwea wakabidhiwa majukumu

**Na Mwandishi Wetu,**
NACHINGWEA

MADIWANI wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, wametakiwa kwenda kusimamia na kuyatafutia ufumbuzi matatizo yaliyopo kwenye maeneo yao ya kazi, kwa vile wao ni kiunganishi kati ya wananchi na serikali.

Wito huo ulitolewa juzi na mbunge wa Nachingwea, Dk. Amandus Chinguile, kwenye kikao cha kwanza cha baraza la madiwani na kusema, kwenye maeneo yao kuna matatizo mengi ambayo serikali inakwenda kuyatatua.

"Diwani ni kiunganishi kati ya serikali na wananchi, hivyo ni kutambua nafasi alionayo na ukubwa wake na kuithamini kwa kwenda kutafutia ufumbuzi matatizo yanayowakabili wananchi," alisema Dk. Chinguile.

Alisema madiwani hawatakiwi kujiona kama wameyapatia maisha, bali watoe ushirikiano na usikivu kwa wakuu wa idara, vitengo vingine pamoja na wananchi bila kuweka matabaka.

Mbunge huyo alisema, matabaka ni sumu ya maendeleo, hivyo madiwani wasiwe chanzo cha kugawa wananchi, bali wawaunganishe na kushirikiana nao katika kutatua matatizo yanayokwamisha maendeleo.

Aliwakumbusha kuwa, wanatakiwa kutumia nafasi zao hizo kujijengea heshima ya utumishi bora na kuleta maendeleo kwenye maeneo yao na hivyo kuifanya Nachingwea kuwa juu kwa maendeleo.

"Lakini nitoe wito kwa wanahabari kwamba, tumieni kalamu zenu vizuri kwa maslahi mapana ya wilaya ya Nachingwea na taifa kwa ujumla ili kuendelea kuwa na amani na umoja wa kitaifa," alisema.

Aidha, kabla ya mbunge kutoa hotuba yake hiyo, madiwani walianza kula kiapo cha utumishi kwa wananchi na pia uchaguzi wa mwenyekiti wa halmashauri ya Nachingwe na makamu wake.

Mbali na uchaguzi wa viongozi hao wa halmashauri, madiwani pia waliunda kamati mbalimbali za kudumu pamoja

# Ekari 170 kutumika maonyesho Nanenane

**Na Vincent Tiganya,** TABORA

MKOA wa Tabora umetenga zaidi ya ekari 170 kwa ajili ya maonesho ya sikukuu za nane nane kitaifa ambayo yanatarajia kufanyika mwakani katika eneo hilo.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philemon Sengati, baada ya kutembelea eneo kwa ajili ya kujionea ukubwa wa eneo na miundombinu mbalimbali iliyopo katika eneo hilo.

Mkuu huyo wa mkoa alisema wameshapata barua kutoka Wizara ya Kilimo ya kuandaa maonyesho ya Nanenane kuanzia 2021 hadi 23 na wako tayari kuwapokea wageni wote watakaoshiriki.

Alisema wanao uzefu wa kuandaa maonyesho kwa kuwa tayari eneo hilo lilianza kutumika kwa maonesho tangu mwaka 2014, na linayo miundombinu ya barabara, umeme, maji na majengo ya kudumu kwa baadhi ya Halmashauri za mkoa huo.

"Tuwakaribisha wote wenye nia ya kuja kuonyesha teknolojia ya kisasa ya ufuagaji na mifugo, na wale wanaofundisha juu ya kilimo biashara wakaribie …tutawapa maeneo ya kuendeshea shughuli hiyo," alisema.

Alisema mazingira ni rafiki kwa kuwa maji ya kutosha kutoka Ziwa Victoria yamefikia, na gharama yake ni nafuu na umeme upo katika eneo kubwa la Uwanja.

Dk. Sengati alizikaribisha wizara, taasisi, Idara, mikoa, kampuni na sekta binafsi ambazo zinataka kushiriki maonesho hayo ya kitaifa kuomba maeneo ya kuwekeza kwa kuwa ardhi ipo ya kutosha.

Alisema Wizara ya Maliasili na Utalii imeshaomba eneo la kuweka miundombinu yake kwa ajili ya kushiriki maonesho hayo.

Dk. Sengati alisema Mkoa huo kwa kushirikiana na Kigoma, wamejianda kuhakikisha maonyesho hayo yanatumika kama darasa kwa wafugaji , wavuvi, wakulima kufanya shughuli kwa kutumia teknolojia ili kuwa na tija.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa ya Tabora, William Mpangala, alisema huduma mbalimbali zikiwamo za matibabu zinapatikana katika eneo hilo kwa karibu na viwanja hivyo wamejenga Kituo cha Afya ambacho kinaendelea na matibabu.




Wanafunzi kutoka shule za sekondari za Manispaa ya Shinyanga, wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali kwenye uzinduzi wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mradi kumaliza adha ya maji Mkuranga

**Na Frank Monyo**

WAKAZI wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani na maeneo jirani, wanatarajiwa kuondokana na adha ya ukosefu wa maji baada ya ujenzi wa mradi wa maji wa zaidi ya Sh. bilioni 2 kufikia asilimia 90 ya utekelezwaji wake.

Kauli hiyo imetolewa na Meneja usimamizi wa mradi huo, Mhandisi Erasto Mwakilulele, alipokuwa akitoa taarifa ya ujenzi wa mradi huo, jana, kwa Mbunge wa Mkuranga Abdallah Ulega, wakati wa ziara yake ya kutembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa wilayani humo.

Alisema matarajio ya wananchi wa wilaya hiyo kuanza kupata maji ni Februari mwakani, baada ya kukamilika kwa ujenzi wa eneo litakalofungwa pampu za kusukuma maji ambao ujenzi wake umefikia asilimia 30 hadi sasa.

"Upande wa tangi la kuhifadhia maji litakalokuwa na uwezo wa kubeba lita za maji milioni moja na nusu, ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 90 na kwamba kinachoendelea kwa sasa ni umaliziaji wa baadhi ya vitu, huku wakisubiri kukamilika kwa ujenzi wa eneo zitakapofungwa pampu," alisema Mwakilulele na kuongeza:

"Matarajio hadi kufikia Februari mwakani kazi hii itakuwa tayari imekamilika na wananchi waanze kupata maji kutoka katika mradi huu," alisema.

Mbunge Ulega, alimtaka msimamizi wa mradi huo, pamoja na mkandarasi kuhakikisha kazi ya ujenzi wa mradi huo inakamilika mapema iwezekanavyo ikibidi hata kabla ya kipindi hicho kufika ili kuondoa adha ya maji inayowapata wananchi.

Alisema kwa jiografia ya Mkuranga, Februari huwa ni kipindi chenye mvua nyingi, hivyo endapo ujenzi huo utacheleweshwa hadi kufikia wakati huo, wananchi wa wilaya hiyo wataendelea kuusubiri kwa kipindi kisichojulikana, suala alilosema hapendi kuona likitokea.

Katika hatua nyingine, Ulega alimwagiza mkandarasi wa mradi huo kuwasilisha ofisini kwake utaratibu wa malipo anaoutumia kuwalipa wafanyakazi wanaojenga mradi huo baada ya uwepo wa malalamiko ya baadhi yao kuhusu malipo hayo.

Alisema hadi kufikia saa 2 asubuhi ya kesho anahitaji taarifa hiyo iwe imefika katika ofisi yake, ili kujua chanzo cha malalamiko hayo.

Mradi wa maji Mkuranga -Vikindu unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) na kutekelezwa kupitia fedha za ndani za mamlaka kwa gharama ya Sh. bilioni 2.2.

# NEMC, TBS wateta na wazalishaji, wasambazaji vifungashio plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya siku kadhaa tangu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), kutoa tamko la kuzuia matumizi ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango vya Shirika la Viwango nchini (TBS) ifikapo Desemba 31, Baraza limekutana na wazalishaji, wasambazaji na wadau wa mazingira ili kuangalia namna nzuri ya kutekeleza tamko hilo bila kuleta athari hasi kwa wahusika.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema mkutano huo umelenga kutoa ufafanuzi wa sheria za mazingira pamoja na kanuni zake ambazo baraza imekuwa ikizisimamia.

"Mwishoni mwa juma lililopita NEMC ilitoa tamko la kuzuia vifungashio ambavyo havikidhi vigezo vya TBS ifikapo Desemba 31, mwaka huu, tamko ambalo lilipokewa vizuri na watu waliowengi. Hata hivyo, tumelazimika kukutana na wazalishaji, wasambazaji pamoja na wadau wa mazingira kuelezana juu ya sheria na kanuni za mazingira na kuangalia namna nzuri ya utekelezaji wa tamko hilo," alisema Dk. Gwamaka.

Dk. Gwamaka alisema NEMC na TBS wamekuwa na kazi ya kusimamia kanuni, sheria na viwango vinavyostahili ili kulinda mazingira ya vizazi vya sasa na vijavyo.

"Tamko letu la wiki iliyopita liliwataka wenye viwanda kuzalisha vifungashio ambavyo viwango vyake vinakubalika na TBS na sifa yake kubwa viweze kurejelezwa pamoja na kuwekwa lebo ili iwe rahisi kumtambua mzalishaji ili kudhibiti usambaaji wa vifungashio hivyo katika mazingira yetu," alisema.

Alisema kuwa Baraza na TBS wametumia nafasi hiyo kutoa elimu na ushauri wa namna ya kufanya ili kuyalinda mazingira ambayo yameathirika pakubwa kutokana na uzalishaji wa holela.

"Vifungashio ambavyo vimekuwa vikitumika huko mitaani ni ngumu kurejelezwa, lakini pia havina lebo jambo ambalo linaondoa usawa wa kibiashara kwa wafanyabiashara ambao wamekuwa wakizalisha vifungashio mbadala kwa kutumia karatasi ambavyo vimekuwa rafiki kwa mazingira na pia wamekuwa wakilipa kodi kubwa serikalini," alieleza Dk. Gwamaka.

Mkurugenzi wa Upimaji na Ugezi kutoka TBS, Mhandisi Johanes Maganga, alisema watahakikisha wanasimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa kwa mujibu wa sheria na watashirikiana na wawekezaji wanapata "certifiacation", na kwamba watafanya kazi kwa karibu na baraza kujua ni wawekezaji gani wamefikia vigezo vilivyoweka pasipo kuathiri uzalishaji wao.

Naye Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara, Abdallah Mwinyi, alipendekeza kuwa wakati sheria na kanuni zinapotungwa, ni vyema kuwahusisha wafanyabiashara wadogo, ambao wamekuwa wakitoa huduma kwa watumiaji wa mwisho.




Ukurasa 12

FOVAC inavyoibua mtaji wa msitu kuanzia Sh. mil 300 za mnyoyoro thamani wa mbao



Ukurasa 14

**Mfuko Uwekezaji wavuka malengo baada ya kombora maradhi corona**


# BUFE

IJUMAA DESEMBA 4, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


# Eat Just, kampuni iliyobuni nyama ya kipekee mwonekano 'kuku fulani'

## • Maswali sokoni; ni tamu na inalipa?

**Na Mwandishi Wetu**



Ndivyo ilivyo nyama hiyo ya 'kuku', zikitarajiwa katika soko la nchini Singapore. **PICHA: MTANDAO**

SHIRIKA binafsi ndani ya Singapore, imeiweka nchi hiyo kuwa ya kwanza duniani kubuni na kuruhusu nyama ambayo haijatokana kwa mnyama aliyechinjwa, kuingia sokoni kutumika, ukifanana kwa sura nyingi na nyama ya kuku.

Unatajwa kuwa uamuzi unaogeuka kuwa mwanya wa kuingiza sokoni mshindani wa kwanza wa nyama halisi ya kuku halisi sokoni, pale watakaponunuliwa na kuliwa na wateja watakaovutiwa nayo, bidhaa hiyo ya maabara, badala ya zilizozoeleka mifugo toka zizini au kwenye mabanda.

Kampuni ya kutengeneza nyama hizo nchini Singapore, hadi sasa haijasema lolote, kuhusu tarehe kamili ya bidhaa hiyo kuanza kutumika sokoni, kwa maana ya ndani ya Singapore.

Ubunifu wa bidhaa hiyo mpya ya nyama, unatajwa ni zao la uhitaji wa mbadala unavyozidi kuongezeka, kutokana na wasiwasi wa wateja juu ya usalama wa afya zao, kutokana na makuzi ya wanyama na mazingira yanayowazunguka.

Wachumi wa kibenki, nao wameshaingia sokoni na kubashiri ukubwa wa soko la nyama mbadala kwamba huenda itafika thamani ya Dola za Marekani bilioni 140 (£104bn) au sawa na Sh. trilioni 322 ndani ya muongo mmoja ujao duninani, ikishika asilimia 10 ya idadi ya viwanda vya nyama duniani.

Kitaalamu, bidhaa hiyo mpya inatajwa kuwa aina ya nyama ambazo katika mazingira ya kawaida hazina uhusiano wowote na mimea, lakini zimekuzwa katika maabara kupitia utaalamu wa aina yake.

Breakthrough, kampuni ya chakula cha viwandani inayozalisha bidhaa hiyo, inaeleza matumaini yake kuwa mataifa mengine yataanza kufanya kile wanachokifanya ndani ya muda mfupi ujao.

Hadi sasa ni zaidi ya muongo mmoja umepita, kumekuwa kufanyika majaribio kadhaa ya kuleta nyama mbadala sokoni, kukibashiriwa matumaini ya kupata walaji wengi zaidi na kuandaa bidhaa bora zaidi.

Katika sura ya kupanuka mkakati, kampeni na hata soko, nchini Israel, kunaelezwa kuwapo matumaini teknolojia ya kutengeneza nyama yenye ladha nzuri na kupata soko la gharama nafuu, ubinfu wake unaaanza kuchukua nafasi.

Wakati wengine wakihisi kuwapo faida katika mazingira hayo,wapo wanasayansi wanaohisi teknolojia hiyo inaweza kusababisha madhara makubwa zaidi katika mabadiliko ya tabianchi duniani.

Mkuu wa kampuni ya 'Eat Just' aliuita uvumbuzi huo kuwa mojawapo ya hatua kubwa muhimu katika sekta ya viwanda vya chakula, lakini katika sura ya pili kuna vikwazo. Kwanza, inatajwa nyama ya 'kuku' hao wa maabara ni ghali zaidi kutengeneza, ikiliganishwa na kuku halisi.

Awali kampuni ya Eat Just, ilisema ingeuza nyama ya kuku wa maabara kwa bei dola 50 (Sh.115, 000) kila mmoja, ingawaje kuna taarifa ya kushuka gharama kwa sasa. Hata hivyo haijatajwa.

Changamoto nyingine kwa kampuni wazalishaji wa nyama ya maabara, ni jinsi kunakuwapo mtihani wa namna bidhaa hiyo inavyopokewa na wateja, ambao pia ndio walaji wenyewe.

Matarajio yanayoelekezwa kisoko, ni kwamba wazalishaji Eat Just na nchi yao ya Singapore, wana nafasi na uwezo wa kuwavutia washindani kuanzisha biashara ya aina hiyo katika maeneo mengine kimataifa, kuchochea uzalishaji na soko kinchi.

### USALAMA WAKE?

Shirika la Vyakula la Singapore (SFA), linaitetea kwamba kikundi cha wataalamu wake walifanya tathmini ya data kuhusu ulaji wa chakula kilichotengenezwa na kampuni ya Eat Just, pia kupima usalama wa kuku wa maabara na ikalitolea maelezo kwamba:

"Ilibainika kuwa, kuku hao ni salama kwa ulaji kwa viwango vilivyokusudiwa kutumiwa na waliruhusiwa kuuzwa nchini Singapore, kama mojawapo ya bidhaa zilitokana na wazo la thamani au za Eat Just," ilisema asasi hiyo.

Shirika hilo la kutathmini linafafanua lilivyofanya kazi hiyo, kwamba liliweka muundo wa udhibiti viwango kwa vyakula vipya kuhakikisha nyama inayotengenezwa maabara na protini nyingine mbadala, zinatimiza viwango stahiki, kabla ya kuuzwa ndani ya Singapore.

"Nina uhakika kwamba uidhinishaji wetu wa nyama inayotengenezwa katika maabara, utakuwa wa kwanza kati ya wengi nchini Singapore na nchi nyingine kote duniani ," anasema Josh Tetrick, Muasisi Mwenza wa Eat Just, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Anasisitiza, hakuna dawa za antibaiotiki zilizotumiwa katika mchakato mzima na kuku walikuwa na kiwango cha chini cha maikrobaiolojia kuliko wa kawaida, ilisema kampuni hiyo.

"Ni nyama ya kwanza duniani kuruhusiwa na wadhibiti wa viwango, nyama yenye kiwango cha hali ya juu iliyobuniwa kutoka kwa seli (chembehai) ya mnyama, kwa ajili ya kuliwa na binadamu, ambayo inatoa fursa ya kuanzishwa biashara za kiwango kidogo nchini Singapore siku zijazo," ilisema kampuni ya Eat Just, katika taarifa yake.

***Makala hii ni kwa taarifa za mitandaoni kimataifa***

BIASHARA

MRADI WA FORVAC

# Namna inavyoibua mtaji wa msitu kuanzia Sh. mil 300 mnyoyoro thamani wa mbao

**Na Christina Haule,** TUNDURU

• Dira Sh. mil 700; imesheheni neema kibao vijijini

KUNA mafanikio kuhusiana na Programu ya Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Misitu Tanzania (FORVAC), ambao mantiki yake ni kuongeza faida kiuchumi, kijamii na kimazingira, kutokana na usimamizi endelevu wa misitu.

Hiyo inafanyika kwa njia ya kuongeza thamani ya mazao ya misitu na kuimarisha maisha ya jamii kwa ujumla, ikizingatia kuendeleza mnyororo wa thamani kwenye mazao ya misitu kama vile mbao, mkaa, asali na nyingine zisizotokana na misitu.

Hadi sasa inaelezwa imeshanunua mashine mbili zinazotembea (mobile conveters) za kuchakata mbao zenye thamani ya Sh.milioni 300 ili kusaidia kukuza mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu kwa vijiji vyenye misitu katika kongani mbili kati tatu zilizopo kwenye wilaya 10 zinakotekelezwa mradi huo.

Alex Juhani Njahani, msimamizi mtaalamu wa misitu kutoka FORVAC, anasema hayo alipokagua miradi hiyo vijijini; Nandenje wilayani Ruangwa, mkoani Lindi na Sauti Moja wilayani Tunduru, Ruvuma, inayofadhiliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na serikali ya Finland.

Pia, Njahani anafafanua mashine zilizogawiwa wilayani Kilwa na Tunduru, zina uwezo wa kuchakata magogo na kutoa mbao zenye ubora, hivyo kuongeza thamani ya mbao sokoni.

Anasema matumizi ya mashine zingine yalichangia hasara ya kupotea mbao nyingi na kuchangia hasara, hivyo kupoteza mnyororo wa thamani katika mazao ya misitu.

"Zamani vijiji viliuza magogo na kupata asilimia 60 pekee. Kupitia mashine hiyo, wanauza mbao ambazo hupata asilimia 60 kwa kila ubao mmoja unaotoka kwenye gogo moja, ambalo hutoa zaidi ya mbao tatu" anaeleza Njahani.

### ZAO LA FUNZO

Njahani anasema, kutokana na mafunzo waliopewa wasimamizi msituni, kuna watu 330,000 walionufaika baada ya fedha zinazopatikana kuingia katika maboresho ya huduma za kijamii kama vile zahanati, madarasa ya shule, kukatiwa bima ndogo za afya (CHF), ujenzi wa ofisi za vijiji vyote vya mradi.

Bwana Miti kutoka Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo wilayani Tunduru, Ruvuma, Yusuph Kiangio, anaushukuru mradi wa FORVAC, kuwapatia mashine hiyo iliyoongeza thamani ya magogo kutoka asilimia 42 hadi 63, malengo ni kufika asilimia 80.




Bwana miti kutoka Shirika la Kuhifadhi Mpingo na Maendeleo wilayani Tunduru, Ruvuma Yusuph Kiangio, akiendesha mashine ya kuchakata mbao wakati ikipasua magogo.

> **Matumizi ya mashine zingine yalichangia hasara ya kupotea mbao nyingi na kuchangia hasara, hivyo kupoteza mnyororo wa thamani katika mazao ya misitu.**



Mratibu wa asasi ya Forviac Taifa, Emmanuel Msofe (kulia), akisikiliza maelezo namna mashine ya kuchakata mbao inavyofanya kazi, ili kukuza mnyororo wa thamani wa mazao misitu. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**

Kiangio anasema, kupatikana mashine hiyo mpya ya kuchakata mbao aina ya Bensor Norwood mwaka jana, kumesaidia kukuza mnyororo wa thamani ya mazao ya misitu, ikijumuisha mbao bora, vipande vya mbao kutokana na ubora, vyote vinapouzwa vinarejesha kipato kwa kijiji husika.

Anaeleza, hivi sasa wanajipanga kuuza mabanzi yanayobakia baada ya mbao kukatwa kutoka kwenye magogo yenye urefu wa mita za ujazo 100, ambazo awali waliuza kwa bei Sh. mil 400, sasa mtazamo ni kuuza Sh. milioni 700, sawa na nyongeza ya asilimia 75.

Mtaalamu Ufundi wa FORVAC Tanzania Juhani Harkonen, anawashauri viongozi wa kamati za usimamizi wa misitu ya vijiji, kutekeleza vyema mradi, sababu unasaidia misitu ya vijiji na kuleta mnyororo wa thamani yake, sambamba na ukuzaji utawala bora kwa kuzingatia sheria za misitu zilizopo.

Harkonen anaeleza imani yake kuwa uwiano kati ya vijiji kusimamia vyema misitu katika kutekeleza mradi na kupatikana matokeo chanya yanayokusudiwa.

### WENYE VIJIJI

Ofisa Mtendaji wa kijiji cha Sautimoja, wilayani Tunduru, Philemon Dustan, anasema wameshaingiza Sh. milioni 118 kupitia mauzo ya magogo, mbao na mianzi kutoka sehemu ya hekta 21,969 za misitu ya vijiji walizozitenga.

Dustan anasema, fedha hizo zinatokana na kuuza mbao baada ya magogo kuchakatwa na kuuzwa kwa wateja mbalimbali na zimetumika kununua pikipiki mbili za Kamati ya Maliasili ya Kijiji, kufanya doria na kazi za msituni.

Pia, anataja pato hilo limetumika kujenga darasa kwenye Shule ya Msingi Sautimoja, kufyatua matofali ya kujenga nyumba ya mwalimu, kulipia CHF za wajumbe 17, huku wakijiandaa kuwakatia bima kaya 280 kijijini na salio la Sh. milioni 28 zitahifadhiwa benki.

Dustan anasema, wameweka utaratibu wa kuwapa wanafunzi madaftari na kalamu na kuchangia chakula shuleni hali inayowasaidia kupunguza utoro na wanafunzi kuhamasika na mahudhurio shuleni, yanayopanda hadi asilimia 92, kutoka 80 iliyokuwapo

Rai ya Ofisa Mtendaji huyo wa kijiji ni kwamba, kuna haja ya kuwatafutia masoko ya kudumu ya mbao, itakayowaondoa kutoka hali walionayo sasa.

Anadokeza hatua ya mafanikio yao, kwamba waliuza mbao za Sh. milioni 75, ikiwa ni sehemu ya Sh. milioni 118 walizokusanya kutoka wateja wa ndani wa misitu, wakiwamo Mfuko wa Wanyamapori Duniani (WWF) waliowatafutia wateja wa kimataifa.

Dunstan, anayeonyesha umakini katika anachofanya kupitia angalizo wa Lengo la Sheria ya Misitu Namba 14 ya Mwaka 2002, inayozuia uvunaji holela wa misitu, badala yake kuwa endelevu.

Pia, anataja kwa sasa wana mpango wa kuweka mizinga ya nyuki 50 katika misitu ya hifadhi ya kijiji hicho, ili iwanifaishe na mazao yake misituni. Glory Msigara, ni Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Msitu wa Kijiji cha Sautimoja, anataja manufaa ya mashine waliopata kutoka mradi wa FORVAC, ni kupata mashine hiyo yenye uwezo wa kujiendesha pasipo kutegemea nguvu kubwa za binadamu na inawapatia faida kubwa za mazao misitu tofauti na mashine ya mkono waliokuwa nayo awali.

Anasema, awali walipasua magogo kati ya mawili na matatu kwa kutumia msumeno wa mkono kwa siku, lakini mageuzi ya sasa ni kupasuliwa magogo kati ya 10 na 15, hata kujenga ushuhuda wa tija kuanzia ngazi vijiji hadi halmashauri inayowaongoza.

### OFISA MISITU

Kaimu Ofisa Misitu Wilaya ya Tunduru, Samson Remmy, anasema changamoto ya masoko walionayo imeshapatiwa ufumbuzi, kupitia Vikao vya Uvunaji Wilaya walivyoangalia idadi ya wavunaji waliopitishwa na kuwaelekeza kuvuna kwenye misitu ya vijiji, ili kuleta maendeleo nyumbani.

Remmy anasema, kupitia mauzo ya thamani hizo za mazao ya misitu, halmashauri imekuwa ikipata asilimia tano inayokwenda kwenye shughuli mbalimbali, ikiwamo doria na ushauri.

Hata hivyo, anasema baada ya kuona manufaa ya mradi wa FORVAC, sasa wanajipanga kuviwezesha vijiji vitatu vilivyoko Tunduru, navyo viingizwe katika neema hiyo.

Ofisa Misitu hivi sasa, anaiomba serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, iendelee kuelimisha jamii, ili fursa zilizopo misituni zidumu na kuleta maendeleo kwenye vijiji.

Mratibu wa FORVAC kitaifa, Emmanuel Msoffe, anataka uongozi wa Kijiji cha Sautimoja kupitia Kamati za Maliasili, kutumia mashine waliyopewa kama kiwanda vidogo, ili kuzalisha bidhaa na hivyo kutekeleza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Maendeleo ya Viwanda

Mradi unatekelezwa katika Kongani tatu ambazo ni: Tanga katika Wilaya za Kilindi, Handeni, Kiteto na Mpwapwa; Kongani ya Lindi programu inatekelezwa katika wilaya za Ruangwa, Liwale na Nachingwea; na Ruvuma kwenye Wilaya zaTunduru, Namtumbo, Songea, Mbinga na Nyasa.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Chonde chonde wateule msiwaangushe wateuzi






NA JOSEPH KULANGWA
(+255) 713 410008
jkulangwa@yahoo.com

ILIKUWA siku nzuri sana kwa Wazanzibari 13 walioapishwa na Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar mpya, Dk. Hussein Ali Hassan Mwinyi katika Ikulu ya Zanzibar.

Waliapishwa kuwa mawaziri katika serikali hiyo ya awamu ya nane, huku wakipewa ajenda 13 za kufanyia kazi waliyoianza siku hiyo ya Novemba 21, bila kuvuta miguu.

Ajenda iliyonivutia ni ya kutakiwa kuwa wabunifu wa mbinu mpya za kuleta ufanisi kiutendaji, huku wakitakiwa pia kutumia wataalamu walionao katika wizara zao.

Walipewa ajenda hizo na Rais, ambaye alionyesha waziwazi kutaka kutimiza ahadi alizozitoa kwa wananchi, alipokuwa akiomba ridhaa ya kurithi mikoba ya Dk. Ali Mohammed Shein.

Nasema ajenda ya ubunifu, ilinivutia zaidi, kwa sababu ndiyo inayoweza kumpima mtu, kama kweli ni kiongozi anayeweza kuongoza wengine, kwa kuja na mambo ambayo wengine hao hawana, katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

Naamini hata Rais Dk. John Magufuli, atakapokuwa amekamilisha uteuzi wa wasaidizi wake, atawaambia kwa lugha hiyo hiyo, yenye ajenda ya ubunifu, ili kuondokana na tabia ya kumsubiri Rais afanye kila kitu.

Ilikuwa wazi katika muhula wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa baadhi ya watendaji kukosa ubunifu na badala yake kumsubiri kiongozi wa nchi afanye kila kitu.

Tulishuhudia katika mikutano yake mingi ya hadhara, akitundikiwa mabango yenye malalamiko kutoka kwa wananchi, huku naye akilazimika kuwasimamisha wasaidizi wake kujibu hoja za kero katika maeneo yao.

Akidhani mwanzoni kuwa kulikuwa na matatizo makubwa yaliyoshindikana, Rais Dk. Magufuli alilazimika kusikiliza ufafanuzi uliotokana na mabango hayo, na kuchukua hatua za papo kwa hapo, hata akawaacha wananchi wameridhika.

Lakini, baadaye alibaini kwamba, kuna mengine yalikuwa yanawezekana kutatuliwa katika ngazi za chini za mikoa, wilaya na hata tarafa, lakini tatizo lilikuwa uzembe tu wa baadhi ya watendaji.

Kuna nyakati alisikika akilalamika kuhusu matatizo ya baadhi ya maeneo kumsubiri yeye, ndipo suluhisho lipatikane! Hiyo kwa vyovyote ilimchosha kama si kumuuma, kwamba wananchi wanateseka huku viongozi wakisubiri ziara zake kupata ufumbuzi.

Huo ni ugonjwa waliokuwa nao baadhi ya wasaidizi wake na pengine bado haujapona na yawezekana ndiyo sababu pia, akachukua muda mrefu kidogo kuunda baraza lake jipya la mawaziri.

Binadamu tunatofautiana uwezo wa kufikiri na kutenda. Wapo wanaoweza kufikiri haraka na kuchukua hatua, lakini wapo wanaojivuta, ama kutokana na hulka tu. Na hao ndio huchelewesha maendeleo.

Wapo viongozi ambao hawawezi kufanya kitu mpaka wamwone mkuu wao amefanya au anasema nini, ndipo nao hujitokeza na kupita nyayo hizo hizo. Hawa ni wasiojiamini na wanaoogopa lawama.

Hawajui kuwa bora kutenda vibaya ulaumiwe, kuliko uchelewe ufedheheke. Kama kiongozi utasubiri kuona mkubwa wako anafanya nini ndipo nawe ufanye, unakuwa huna sababu ya kuwa ulipo.

Hali kadhalika, kuna viongozi unaoshindwa kuwasoma wakuu wao na kudhani wanachokifanya kitawafurahisha, lakini kumbe ni kinyume chake na hujikuta wakiharibu. Hao nao hawafai.

Madaktari Magufuli na Hussein ni binadamu, wanaweza kuteua watu wakiamini na kuwaamini kuwa wanaweza, lakini wateule wakajikuta wameharibu na kuwafedhehesha, lakini kama alivyoahidi Dk Hussein: "Waziri ukishindwa kushughulikia hayo, maana yake hunifai…ukifanya vizuri utabaki na ukifanya vibaya utaondoka."

Maana yake hapo anazungumza lugha ya kaka yake ya Kutumbua Majipu, aliyoifanya ya kikamilifu katika muhula wake wa kwanza. Nadhani safari hii hataki atumbue, amechoka 'kurukiwa usaha', ndiyo sababu anafanya umakini mkubwa.

Ni vyema kuchelewa ufike kuliko kuwahi ukaishia njiani. Tumewaona wa Dk. Hussein, tuwaone sasa wa Dk. Magufuli. Inshallah, tunasubiri muhula wa kwanza wa Dk. Hussein na wa pili na wa mwisho, wa Dk Magufuli. Alamsiki!

UCHUMI

# Mfuko Uwekezaji wavuka malengo baada ya kombora maradhi corona

• Mwenyekiti asema wameweka historia • Siri? Mitandao simu yailetea maajabu




Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, akizungumza na wawekezaji mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, alipozindua mikutano wa mwaka ya mifuko ya uwekezaji inayoziendesha. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu, Simon Migangala na kushoto ni Mjumbe wa Bodi hiyo, Francis Chacha. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

**Na Frank Monyo**

MBALI NA na matatizo ya ugonjwa Covid-19 katika mwaka wa fedha ulioisha Juni 30, Mfuko wa Dhamana ya Uwekezaji (UTT) unajigamba bado ni mkubwa na umeongezeka kwa asilimia 42, mageuzi yalioyopigwa baada kupungua kwa asilimia 1.5 mwaka uliopita.

"Pamoja na changamoto za ugonjwa wa Covid- 19 na mabadiliko ya sera za uwekezaji katika nchi zinazoshirikiana na Tanzania, utendaji wa soko bado umeendelea kuwa wa kuvutia na kuridhisha," anasema Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Casmir Kyuki.

Ni kauli yake kwenye Mkutano Mkuu wa 12 wa Wawekezaji wa mfuko huo, jijini Dar es Salaam hivi karibuni, akijivuna kuwapo hatua ya viashiria vya soko na utendaji wa mifuko yake hadi Juni 30, mwaka huu, umepiga hatua.

"Ukubwa wa mifuko ya uwekezaji iliongezeka kutoka Sh. bilioni 290.7 Juni 30,2019 hadi Sh. bilioni 412.8 Juni 30, 2020," anasema Kyuki na kuendelea:

"Ongezeko hili la Sh. bilioni 122.1, sawa na asilimia 42 ukilinganisha na kupungua kwa Sh. bilioni 4.4 sawa na asilimia 1.5 hasi kwa mwaka uliopita,"

Anafafanua kukua kwa mifuko ndani ya mwaka mmoja uliofikiwa kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa mifuko ya uwekezaji wa UTT AMIS, pamoja na taasisi zilizoitangulia.

> **Juhudi zinafanyika kuhakikisha kuwa teknolojia zilizopo zinakusanywa, kuzalishwa, kuboreshwa na kutumika kitaaluma kwa ajili ya maendeleo ya taifa.**

Kyuki anataja viashiria vya kuongezeka idadi ya wawekezaji 13,671 sawa na asilimia 9.4 ikilinganishwa na ongezeko la wawekezaji 5,169 sawa na asilimia 3.7 mwaka uliopita. Lingine analitaja ni pato la UTT kwa ujumla liko vizuri sana na mwenyekiti huyo anazitaja pamoja na kiwango katika mabano ni: pato kwa wawekezaji ni asilimia 10.3, Mfuko Bond (16.2%), Liquid (15.1%), Jikimu (15.6%), Wekeza Maisha (24%) na Watoto (12.7%).

### MAFANIKIO YAKOJE?

Kyuki, anataja mafanikio ya UTT AMIS yameongezeka maradufu kufikia wastani wa Sh. milioni 300 kwa mwezi, baada ya kuzinduliwa huduma hiyo kupitia njia ya simu.

"UTT AMIS inajivunia ongezeko hili kwani ni zuri, hata hivyo kampuni itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu huduma kwa njia ya mitandao ya simu kwa kuwa tunaamini bado kuna fursa ya kuongeza miamala zaidi ya hapo tulipofikia," anasema.

Kyuki anasema, matumizi ya mitandao simu yamerahisisha wawekezaji kujiunga nayo, mara tu huduma ilipozinduliwa. Anaisifu serikali ilivyotaua haraka janga corona, hali iliyofungulia njia mafanikio ya leo.

Mwenyekiti huyo anasema, katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, faida ya mfuko ilikuwa asilimia 10.3, ikiwa ni zaidi ya kigezo linganishi kilichokuwapo.

Kyuki anafurahia kwamba UTT inaendelea kukua na kuvutia wawekezaji kutokana na kuongezeka imani ya wawekezaji wake. Anataja vigezo vya kukua mfuko, ni pamoja na elimu inayotolewa na meneja wake kuhusu faida za uwekezaji wa pamoja.

### UCHUMI, SOKO, FEDHA

Kyuko anasema viashiria vya kiuchumi vinaonyesha uchumi wa Tanzania unaendelea kukua, akifafanua: "Sekta za Ujenzi, Kilimo, Usafirishaji na Madini ambazo kwa pamoja vilichangia asilimia 60 ya pato ghafi la Taifa ziliongoza kwa ukuaji, kwa mujibu wa Shirika la Takwimu la Taifa (NBS), mfumuko wa bei ulibaki kuwa asilimia 3.2 mnamo Juni 30, 2020," anasema Kyuki.

Anaongeza kuwa, takwimu za Benki Kuu kupitia jarida la uchumi linaonyesha hadi Juni 30, mwaka huu, thamani ya shilingi ya Tanzania ilimarika, dola Marekani ikiuzwa kwa thamani ya Sh. 2300.

### HUDUMA MPYA

Pia, Mkurugenzi Mkuu wa UTT AMIS, Simon Migangala, katika halfa hiyo, alizundua huduma ya kusimamia fedha kwa ajili ya wawekezaji wenye kipato kikubwa.

Migangala anasema ni huduma inayolenga kuwezesha wawekezaji au taasisi kuwekeza katika maeneo mahussi, kulingana na matakwa yao.

Pia ana ufafanuzi kwamba ni huduma inayoanzishwa kukidhi mahitaji maalum ya wawekezaj, ambayo hayapatikani katika mifuko mingine ya uwekezaji na inayoendeshwa na asasi hiyo.

"Huduma hii ilikuwa inatolewa kwa wawekezaji mbalimbali kabla ya uzinduzi na mpaka sasa ina kiasi cha Sh. bilioni 16," anasema Migangala.

"Moja ya malengo ya UTT AMIS ni kuendeleza na kubuni bidhaa na kutoa huduma zinazokidhi mahitaji mbalimbali ya wawekezaji katika masoko ya fedha na mitaji hapa nchini ili kuendelea kuwa mshirika hakika katika uwekezaji," anafafanua.

Kimsingi, UTT AMIS iko chini ya Wizara ya Fedha na Mipango, ikisimamia mifuko sita iliyokwishatajwa awali.

### FAIDA ZA UWEKEZAJI

Migangala anataja faida hizo nio kupata mapato na Ukwasi kwa kuzingatia aina ya uwekezaji, kupewa utaalamu wa uwekezaji utakaotatua na kuhusisha mahitaji ya pesa na uwekezaji kwa ufanisi.

Mengi anataja, ni kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji na kupata taarifa ya uwekezaji kulingana na mahitaji yaliyopo na wanaoruhusiwa, ikitoa fursa kwa Watanzania wote, taasisi na wakazi wa Afrika Mashariki.

"Pamoja na kuzindua huduma hii ya 'UTT AMIS - Wealth Management Services, UTT AMIS' inaendela kuwekeza katika mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha wawekezaji waliowekeza kwenye mifuko kupata taarifa za uwekezaji kwa njia ya simu za kiganjani," anafafanua mkurugenzi huyo,

### MATARAJIO YALIYOPO

Migangala anaeleza kwamba wataendelea kutekeleza vipaumbele vya mpango mkakati walio nao. Anafafanua:" Bodi ya Wakurugenzi iliidhinisha kufunguliwa kwa vituo vya huduma kwa wawekezaji katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Mbeya pamoja na Zanzibar.

"Hivyo, mpaka mwisho wa mwaka wa fedha ujao, UTT AMIS itakuwa katika mikoa sita ikijumuisha ofisi za Dar es Salaam na Dodoma. UTT AMIS inawakaribisha sana ili muweze kupata huduma katika ofisi hizo punde zitakapokuwa zimekamilika."

Anawakumbusha wawekezaji na wananchi kwa ujumla kuendelea kutumia mitandao ya simu ili kupata huduma za UTT AMIS kwa mifumo wa mawasiliano walio nayo





Mbunge wa Jimbo la Chamwino, Deogratius Ndejembi (kwenye pikipiki), akisalimiana na wananchi Kijiji cha Ikoa, ikiwa ni ziara yake ya kwanza kukagua miundombinu ya barabara jimboni humo, mkoani Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Shirika laelekeza nguvu kuondoa njaa na umaskini

**Na Ibrahim Joseph,** CHAMWINO

MTANDAO wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali Chamwino (CHANGONET), umejipanga kupambana na njaa na umaskini kwa wakazi wa wilaya hiyo kwa kuanzisha programu ya kilimo cha kisasa.

kwa kushirikiana Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa CHANGONET, Elizabeth Msuya, alisema mpango huo unalenga kuwainua wakulima katika matumizi ya mbegu bora na teknolojia.

Msuya alisema katika kufanikisha azma hiyo, wameanza kutoa mafunzo ya kilimo pamoja na kutoa mbegu bora kwa wakulima kwenye eneo hilo.

Alibainisha kuwa wakulima wengi katika eneo hilo bado wanatumia mbegu duni za mazao jambo ambalo linasababisha kupata mavuno kidogo.

Shirika hilo linalenga kuwafikia wakulima kwa asilimia 90 ndani ya wilaya hiyo ili kuinua kilimo chao na kwamba hatua hiyo inazingatia kuwakutanisha wakulima na wataalamu wa kilimo kutoka TARI ili kupata mwamko wa kilimo. Aidha, alisema wataalamu hao watasaidia upimaji wa mchanga katika maeneo ya kilimo ili kujua aina ya mazao mazao yanayostahili kupandwa.

"Pia wataelimishwa wakulima kuhusu matumizi ya aina za dawa zitakazotumika na zilizopendekezwa ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa,"alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na hali ya hewa ya ukanda wa kati wakulima wanahitaji kuelimishwa kuachana na kilimo cha mazoea na kulima mazao yanayostahimili ukame.

Aliyataja mazao hayo yanayostahimili ukame kuwa ni uwele, mtama, alizeti ,ufuta, mahindi yanayochukua muda mfupi ,karanga na njugu mawe.

MTANDAO wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali Chamwino (CHANGONET), umejipanga kupambana na njaa na umaskini kwa wakazi wa wilaya hiyo kwa kuanzisha programu ya kilimo cha kisasa. Mpango huo unatekelezwa kwa kushirikiana Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI).

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa CHANGONET, Elizabeth Msuya, alisema mpango huo unalenga kuwainua wakulima katika matumizi ya mbegu bora na teknolojia.

Msuya alisema katika kufanikisha azma hiyo, wameanza kutoa mafunzo ya kilimo pamoja na kutoa mbegu bora kwa wakulima kwenye eneo hilo.

Alibainisha kuwa wakulima wengi katika eneo hilo bado wanatumia mbegu duni za mazao jambo ambalo linasababisha kupata mavuno kidogo.

Shirika hilo linalenga kuwafikia wakulima kwa asilimia 90 ndani ya wilaya hiyo ili kuinua kilimo chao na kwamba hatua hiyo inazingatia kuwakutanisha wakulima na wataalamu wa kilimo kutoka TARI ili kupata mwamko wa kilimo.

Aidha, alisema wataalamu hao watasaidia upimaji wa mchanga katika maeneo ya kilimo ili kujua aina ya mazao mazao yanayostahili kupandwa.

"Pia wataelimishwa wakulima kuhusu matumizi ya aina za dawa zitakazotumika na zilizopendekezwa ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa,"alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na hali ya hewa ya ukanda wa kati wakulima wanahitaji kuelimishwa kuachana na kilimo cha mazoea na kulima mazao yanayostahimili ukame.

Aliyataja mazao hayo yanayostahimili ukame kuwa ni uwele, mtama, alizeti ,ufuta, mahindi yanayochukua muda mfupi ,karanga na njugu mawe.

# 'Hakuna atakayekosa fidia mradi wa bwawa'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema itahakikisha kila mwananchi aliyepisha mradi wa bwawa la Farkwa anapata haki yake anayostahili.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Nadhifa Kemikimba, aliyasema hayo jana alipokutana na wananchi wa vijiji vya Bubutole na Mombose kujadili utekelezaji wa mradi huo na kushughulikia malalamiko yao kuhusiana na fidia.

Mhandisi Kemikimba aliwaomba wananchi hao kuwa na subira wakati malalamiko yao yakishughulikiwa na kwamba hadi sasa malalamiko ya wastahiki zaidi ya 400 yamewasilishwa katika mamlaka husika.

Alifafanua kuwa malalamiko yamechukua muda mrefu kushughulikiwa kutokana na kufanya majumuisho ya majibu na wananchi kuwasilisha malalamiko nyakati tofauti.

"Natambua moja ya hoja ziliwowasilishwa ilikuwa baadhi yenu hamkuwa mnaonekana kwenye jedwali la fidia la awali na wengine malipo yenu yalikuwa pungufu.

Hoja hizi zote zimeshughulikiwa na jedwali la nyongeza la fidia limeandaliwa," alisema.

Kadhalika, alisema uthamini wa mali za wastahiki lilifanyika na Sh. bilioni 7.7 zilitengwa kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha eneo la ujenzi wa bwawa hilo.

Alisema watu 2,769 kati ya 2,868 wamelipwa sawa na asilimia 96.5 ya malipo yote na mpaka sasa fedha zilizobaki ni Sh. milioni 213.7 kwa ajili ya watu 100 ambao bado hawajalipwa.

Novemba 21, mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alifanya ziara katika vijiji vya Bubutole na Mombose na kuwahakikishia wananchi kwamba hawatahamishwa mpaka miundombinu ya huduma za kijamii katika sehemu wanakohamia kukamilika.

# Wizara yahamasisha ulipaji kodi mitaani

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeanza utaratibu wa kumilikisha ardhi kwenye mitaa mbalimbali nchini ili kuhamasisha ulipaji kodi ya ardhi na tozo nyingine.

Mkuu wa Kitengo cha Kodi wa Wizara hiyo, Dennis Masami, jana wakati akihamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi na tozo nyingine zinazohusiana na sekta hiyo alipotembelea Mtaa wa Miganga uliopo Ofisi ya Mtendaji Kata ya Mkonze Jijini Dodoma.

Alisema katika kuhamasisha ulipaji kodi ya ardhi na tozo nyingine zinazohusiana na sekta hiyo nchini Wizara imeanzisha utaratibu huo ikiwa ni kusogeza huduma karibu na wananchi.

Akizungumza katika Ofisi ya Mtendaji alisema sasa Wizara imeona umuhimu wa kushusha huduma za ardhi katika ngazi ya mitaa kwa kushirikisha watendaji wa mitaa ili kusaidia utoaji elimu na ukusanyaji maduhuli ya serikali kwa upande wa kodi ya ardhi.

Aidha alibainisha watendaji wa Kata nchini ni muhimu katika kuhamasisha wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya ardhi kwa kuwa wapo karibu na wananchi.

"Wizara imeona ni vizuri ikawatumia kwa ushirikiano na watendaji wa sekta ya ardhi katika halmashauri za wilaya na majiji ili kurahisisha zoezi hili,"alisema.

Aliwahakikishia wamiliki wa ardhi wanaofika wanapatiwa ankara za malipo na kulipia papo hapo kwa taasisi za kibenki ambazo zitakuwepo katika mitaa husika.

"Suala la kusogeza huduma za ardhi kwenye mitaa litawapunguzia gharama wananchi na kuwafanya kuiona serikali inawajali, kupeleka watendaji kumi kwa ajili ya kuhudumia watu 500 katika mtaa inasaidia sana kwani hawatakuwa na ulazima wa kuzifuata huduma mbali," alisema Masami.

Mmoja wa wananchi waliofika kupata huduma kwenye mtaa wa Miganga, Benadicta Kimario, aliipongeza Wizara kwa uamuzi wake wa kusogeza huduma karibu na wananchi na kuelezea uamuzi huo kuwa utasaidia kuondoa kero waliyokuwa wakiipata kufuata huduma ya kumilikishwa na huduma nyingine katika Ofisi za Jiji.

"Mimi nikiwa mjini nilipata taarifa kuwa Wizara imesogeza huduma kwenye mtaa hivyo nikaona nije kuonana na wahusika maana nina kiwanja nataka kuanza kujenga na hapa nimeonana na wahusika na kuhudumiwa, kwa kweli suala hili ni zuri sana," alisema.





## TASAF yaziondoa hofu jamii zisizohakikiwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF), umesema kaya zote maskini ambazo hazikufikiwa kwa sababu mbalimbali katika uhakika wa mzunguko wa kwanza sasa zitafikiwa baada ya mpango huo kuamua kurudia kwenye maeneo yaliyokwisha pitiwa.

Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Lugembe Buyamba, akizungumza juzi na Nipashe baada ya kutoa mafunzo elekezi kwa wawezeshaji wa mfuko huo, alisema zipo baadhi ya dosari zilijitokeza katika mzunguko wa kwanza wakati wa kuandikisha kaya masikini kwa kutofikiwa, wengine kutojitokeza kabisa.

Alisema awamu hii inakwenda kuhakiki na kuwaingiza wote kwenye mpango huo kwa kuhakikisha timu inafanya kazi kwa umakini mkubwa pia waliokuwa katika mpango awali na kutoka awamu hii pia wataingizwa tena.

"Mbali na kula viapo vya uaminifu wawezeshaji hawa pia kazi kubwa watakayoifanya ni kwenda kufanya uhakiki wa taarifa za wanufaika wa TASAF na kuwaingiza kwenye mpango wale wote waliokuwa wamesahaulika na ili kufanikisha hayo lazima wapate ushirikiano kutoka kwa wajumbe wa serikali ya vijiji ambao ni watu watatu," alisema Buyamba.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Mbarali, ambaye ni sehemu ya wawezeshaji katika mpango huo, John Msechu, alisema kuwa utaratibu uliokuwa unatumika awali haukuzingatia jiografia ya Wilaya ya Mbarali kuwa walikuwa wanapangiwa kutembelea vituo kwa muda maalum bila kuzingatia suala hilo.

Alisema baadhi ya watendaji wa vijiji walikuwa hawatoi taarifa sahihi kwa walengwa wa TASAF hali iliyosababisha baadhi hayo kutopata fedha.

Mratibu wa TASAF wilayani humo, Zabron Abel, alisema kabla ya uhakiki walengwa walikuwa 10,318 baada ya zoezi la uhakiki kufanyika walikuwa ni 7,902.

Ofisa Ufuatiliaji mikoa ya Nyanda za Juu kusini, Moris Momba, alisema lengo kuu la mafunzo hayo ni kusaidia wawezeshaji kufanya uhakiki kwa kutumia teknolojia ya vishikwambi ambavyo vitarahisisha kazi na kuokoa gharama.

Alisema wakati wa zoezi la uhakiki wa awali kulikuwa na vikwazo ikiwamo kukosekana kwa umakini ambavyo viliwakwamisha wawezeshaji katika suala la ujazaji wa madodoso.

# Taasisi za umma zadaiwa zaidi ya bil. 2/- maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAMLAKA ya Maji na Usafi wa Mazingira Mbeya, imezilalamikia baadhi ya Taasisi za umma kushindwa kurejesha madeni waliyojilimbikizia ambayo hadi sasa yanafikia Sh. bilioni 2.3 hali inayokwamisha shughuli za utendaji ndani ya mamlaka hiyo.

Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo, Ndele Mengo, alitoa kauli hiyo jana wakati akitoa taarifa ya hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Mamlaka ya Mji mdogo Mbalizi kwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya mjini, Dk. Tulia Ackson, ambaye pia ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania.

Mengo alisema baadhi ya taasisi za umma hazijalipa bili za maji kwa wakati hali inayokwamisha uboreshaji wa huduma za maji kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

Alizitaja taasisi hizo kuwa ni Jeshi la Magereza, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Polisi na kwamba hadi kufikia mwezi Septemba mwaka huu, deni hilo limefikia Sh. 2,363,000,000.

"Mamlaka ya Maji inafanya miradi kwa kutegemea fedha zake za ndani, serikali pamoja na wadau wengine sasa ili kukamilisha miradi mingine ambayo inahitaji fedha nyingi tunahitaji bili za maji kulipwa kwa wakati, tunakabiliwa na tatizo kubwa la bili kutolipwa kwa wakati tunaomba mbunge wetu kwa cheo chako utusaidie kushughulikia hili," alisema Mengo.

Katika hatua nyingine, Mengo alisema hadi sasa jumla ya wateja 87 wasiojiweza wameunganishiwa bure huduma ya maji na cha uniti tano kila mwezi zinatolewa kwa ajili yao ili kuhakikisha wanapata huduma hiyo.

Alisema hadi sasa mamlaka hiyo ina jumla ya mitambo 11 ya kutibu na kusafisha maji na saba kati ya hiyo hufanya kazi ya kusafisha na kutibu maji katika maeneo ya Swaya, Iziwa, Lunji, Mwatezi na Iduda huku mingine minne, Nzovwe, Iyela, Nsalaga na Nsoho ikifanya kazi ya kutibu maji na yote ina uwezo kwa kuzalisha lita milioni 40 kwa siku.

Alitaja moja ya tatizo linalowakabili kwa sasa kuwa ni uharibifu wa vyanzo vya maji na kiasi cha maji kilichokadiriwa wakati wa usanifu katika vyanzo vya maji kilikuwa lita milioni 51, lakini kutokana na uharibifu kwenye vyanzo vya upatikanaji umepungua kufikia lita 40 huku hitaji likiwa ni lita milioni 70 kwa siku.

Akizungumzia suala hilyo, Mbunge Dk. Tulia alisema baada ya Bunge la mawaziri kufanyika atafanya utaratibu wa kukutana na wenye mamlaka hizo ili kufikisha suala la taasisi hizo kudaiwa bili za maji.

Aliiomba Mamlaka hiyo kuwa na uvumilivu kusubiri mchakato wa kuwapata mawaziri na atakwenda kufanya mazungumzo na mawaziri wenye mamlaka ili kulitatua tatizo hilo ambalo linakwamisha utendaji wa mamlaka katika kuwahudumia wananchi.

Kuhusu suala ya uharibifu wa vyanzo vya maji, aliwashauri viongozi kuwapa mamlaka viongozi wa kimila kuhamasisha utunzaji wa vyanzo vya maji na upandaji miti na kueleza kuwa wazee hao ndio wanafahamu vizuri mazingira yao na ni rahisi kudhibiti vitendo vya uharibifu wa mazingira.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Mbeya, Mhandisi Ndele Mengo (kulia), akitoa maelezo kuhusu mradi wa chanzo cha maji cha Nzovwe, unavyofanya shughuli za kuzalisha na kutibu maji, kwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson (mwenye miwani), alipofanya ziara ya kukagua vyanzo vya maji jimboni humo juzi. Wengine ni viongozi wa bodi wa Mamlaka hiyo. **PICHA GRACE MWAKALINGA**

# Ugonjwa mtoto wa jicho tatizo Mbarali

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

ASILIMIA kubwa ya wagonjwa wa macho katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wanasumbuliwa na mtoto wa jicho kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo umri mkubwa na wengine kutotambua dalili mapema ili kutibu ugonjwa huo.

Daktari wa macho katika Hospitali ya Wilaya ya Mbarali ambaye pia ni Mratibu, Dk. Rehema Bidaga, aliyasema hayo juzi wakati wa kuhitimisha kampeni ya upimaji wa macho bure ambayo ilifadhiliwa na taasisi ya Bilal Muslim.

Dk. Bidaga alisema tatizo la mtoto wa jicho linasumbua watu waliofikisha umri wa kuanzia miaka 60 na katika kampeni hiyo pia walitoa huduma za upasuaji.

Alisema jumla ya wagonjwa 50 walipatiwa huduma ya upasuaji wa mtoto wa jicho bila gharama yoyote kwa ufadhili wa taasisi ya Bilal Muslim kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Wilaya.

"Moja ya sababu ya wazee wengi kupata saratani ya mtoto wa jicho ni kuwa na magonjwa nyemelezi pamoja na yasiyoambukiza, pia kutozitambua dalili za awali kuhusu ugonjwa huo, ndio maana katika kampeni hii tukimpima tu akigundulika anaenda kufanyiwa upasuaji siku hiyo hiyo," alisema Dk. Bidaga.

Alisema zoezi hilo limekuwa na mwitikio mkubwa kwa sababu wananchi kutoka kila maeneo ya wilaya walifika hospitalini hapo kufanya uchunguzi wa macho na wameomba zoezi hilo liwe endelevu kwa sababu limeokoa gharama za matibabu.

Aliongeza kuwa sababu nyingine wazee wengi kupata saratani ya mtoto wa jicho ni kushindwa kumudu gharama za matibabu kutokana na hali za maisha.


Baadhi ya wananchi waliopata huduma hiyo, Mwanyanje Deo, mkazi wa Ilemi, alisema taarifa za kutolewa kwa huduma hiyo alizipata kwa jamaa zake.

Alisema tatizo la macho limemsumbua kwa miaka mitatu na alilazimika kufunga safari hadi Mbarali kupata huduma hiyo.

Alisema alizunguka katika hospitali mbalimbali kupata matibabu, lakini hakufanikiwa kutokana na gharama kuwa kubwa na alipofika katika hospitali ya Mbarali alipata vipimo vyote bila gharama hadi upasuaji.

Aliiomba serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kuendelea kutoa huduma bure za matibabu ya macho kwa wazee na makundi mengine kwa kuwa matatizo ya hayo yanachangia kuzorotesha nguvu kazi na uzalishaji kwa wategemezi wa familia.





Meneja Uendeshaji Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP), Jeremiah Mallongo (kushoto), akikabidhi msaada wa vifaa kinga kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Juma Salum Mbwana, katika ofisi za wizara Mnazi Mmoja, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Pili awageukia watendaji taasisi za umma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema watendaji wa taasisi za umma bado wana wajibu wa kuendelea kutekeleza majukumu yao licha ya changamoto wanazopambana nazo katika maeneo yao ya kazi.

Alisema ufinyu wa vitendea kazi, ubovu wa maeneo ya kazi kwa baadhi ya ofisi pamoja na bajeti ndogo wanazopata katika uendeshaji wa ofisi katika taasisi hizo isiwe kikwazo cha kuwapunguzia uwajibikaji wao katika majukumu waliyopangiwa na taifa.

Aliyasema hayo jana wakati akiwa kwenye ziara za kutembelea taasisi zilizo chini ya ofisi yake kukagua uwajibikaji na changamoto za watendaji Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, Chukwani pamoja na Tume ya Ukimwi Zanzibar, Shangani. Alisema Serikali ya Zanzibar imeamua kupunguza matumizi yasiyo na msingi ili kinachokusanywa kifanikishe miradi mingine yenye umuhimu wa kuhudumia jamii kama ilivyoahidi wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu zilizopita.

Aliwataka watendaji wanaosimamia ununuzi wa vifaa na huduma za ofisi wawe na hadhari ya kuepuka mitego ya baadhi ya wafanyabiashara wenye tabia ya kuuza vifaa vibovu visivyo na hadhi ya kiofisi.

Alisema wapo baadhi ya watendaji kwa kushirikiana na wafanyabiashara wajanja huingia kwenye mikataba mibovu ya ununuzi wa vifaa na zana za ofisi matokeo yake fedha nyingi zinazotengwa na kutolewa na serikali kwa kazi hiyo zinaingia mifukoni mwa wajanja hao.

Hemed alibainisha kwamba yapo matumizi mabaya ya fedha ndani ya baadhi ya taasisi za serikali na kusababisha mazingira yasiyokubalika ya ukusanyaji wa mapato jambo ambalo serikali halitalifumbia macho na italazimika kuchukuwa hatua.

Aliwapongeza viongozi na watendaji wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Tume ya Ukimwi Zanzibar kwa uchapakazi wao wa kizalendo bila ya kujali ufinyu wa Ofisi zao kulingana na majukumu yao.

Alisema serikali inatafakari kuwa na azma ya kujenga jengo kubwa litakalokidhi mahitaji ya taasisi na idara zake zote zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar ili kuondoa tatizo la ufinyu wa maeneo ya kazi. Hemed alisema suala hilo muhimu liko kwenye uangalizi wa namna linavyoweza kuchukuliwa hatua inayofaa kulingana na hali halisi ya upatikanaji wa nguvu za utekelezaji.

Akigusia suala la haki za wafanyakazi, Makamu wa Pili huyo aliwataka wakuu wa idara na taasisi za umma kuhakikisha kwamba maslahi ya watendaji wao yanapatikana kwa wakati muafaka.

Alisema haki ya mfanyakazi lazima iheshimiwe na pale inapopungua au kukosekana kwa wakati muafaka, uongozi una wajibu wa kufanya mazungumzo ya busara na mtumishi husika ili kuepuka malalamiko yanayoweza kukwaza uwajibikaji kwa mfanyakazi. Naye Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Issa Mselem, alisema uongozi wa Baraza hilo hivi sasa uko katika hatua ya kuufanyia marekebisho ukumbi wa Baraza hilo ili uendelee kutoa huduma katika kiwango kinachokubalika.

Raya alisema mrejesho wa sauti wakati wa vikao vya Baraza la Wawakilishi vinapokuwa vikiendelea ni tatizo linalofanyiwa marekebisho kwa vile lilikuwa likileta usumbufu kwa wajumbe na wanahabari.

Alisema marekebisho hayo ya sauti ndani ya ukumbi huo yanakwenda sambamba na matengenezo ya paa la jengo hilo ili kuondoa hitilafu inayotokana na maji ya mvua. Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Dk. Ahmed Mohammed Khatib, alisema Tume hiyo imepewa majukumu matano katika utekelezaji wake akiyaainisha kuwa ni pamoja na rasilimali, sera, uratibu, kuzijengea uwezo sekta, kutoa taarifa pamoja na elimu ambayo yamepata mafanikio makubwa.

# UNDP yakabidhi vifaa tiba Wizara ya Afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto imepokea vifaa tiba kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), vitakavyosaidia kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Akikabidhi vifaa hivyo jana, Meneja Uendeshaji wa UNDP, Jeremiah Mallongo, katika Ofisi ya Wizara hiyo huko Mnazimmoja, alisema wanatambua juhudi kubwa za Serikali ya Zanzibar katika kupanga, kuratibu na kutekeleza mpango wa tahadhari kukabiliana na magonjwa hayo.

Alisema vifaa hivyo vitasaidia kupambana na kudhibiti maradhi ya kuambukiza ambayo yanarudisha nyuma soko na mfumo wa utalii na kudhorotesha biashara hiyo muhimu ya kukuza uchumi wa nchi. Alisema vifaa hivyo vina thamani ya Sh. 271,504,378 na pia shirika hilo litagharamia ufungaji wa vifaa tiba vyote katika sehemu ambazo wizara itaamua vifungwe baada ya uainishaji wa maeneo hayo utakapofanyika.

Alisema pamoja na changamoto za upatikanaji wa vifaa hivyo duniani kutokana na mfumuko wa mahitaji makubwa kwa vile kila nchi ikivihitaji vifaa hivyo na kusababisha kuzidiwa uwezo viwanda vya uzalishaji, juhudi kubwa za ufuatiliaji zilifanyika na kuvipata. Alisema ni furaha na heshima kwake kuwasilisha vifaa hivyo ambavyo vimezingatia mahitaji katika kukabiliana na maafa ya kiafya.

"Utakumbuka kwamba, mara tu baada ya maradhi ya maambukizi ya corona kuanza huko katika Jimbo la Wuhan, nchini China, haikuchukua muda maradhi hayo yalisambaa katika mabara ya Asia, Ulaya, Marekani na Afrika, Tanzania ikiwamo Zanzibar pia ziliathirika na wananchi wa Zanzibar soko na mfumo wa utalii uliathirika na hivyo kusababisha kudorora kwa biashara ya utalii," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu ambaye pia Mkurugenzi Tiba wa Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Juma Salum Mbwana, alisema wamepokea msaada wa vifaa hivyo na kuhakikisha watavitumia vizuri kwa lengo la kujikinga na magonjwa mbalimbali ili wananchi waishi katika hali ya salama na amani.

## Watendaji Wizara Elimu watakiwa kubadilika kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said, amewataka watendaji wa wizara hiyo kufanya kazi kwa mujibu wa sheria za kazi na kwenda kwa kasi ya mabadiliko ya kiuchumi ya nchi.

Akizungumza juzi katika mwendelezo wa ziara zake ya kukagua idara na taasisi mbalimbali ziliopo chini ya wizara hiyo, alisema kila mfanyakazi ahakikishe anawajibika katika majukumu yake ili kufikia malengo ya kuendelea kuboresha sekta ya elimu nchini.

Simai alisema muda umefika kwa watumishi wote wa wizara hiyo kuwa wabunifu katika majukumu yao ili kuhakikisha sekta ya elimu inaendelea kupiga hatua katika utoaji wa elimu bora kwa watoto.

Aliwataka watendaji wote kuacha uzembe wakati wa kutoa huduma kwa jamii ili kuendana na kasi ya maendeleo ya serikali ya awamu ya nane.

Hata hivyo, alisema anawajibu wa kuhakikisha anapambana na aina zote ubadhirifu wa mali za serikali na mali za umma na atahakikisha kila mwananchi na mfanyakazi wanapata haki yao kwa wakati.

Alisema anatambua kuwa idara zake pamoja na taasisi mbalimbali zinakabiliwa na chagamoto mbalimbali na amewaahidi watendaji hao kuzitafutia ufumbuzi kadiri hali itakavyoruhusu.

Simai aliagiza kitengo cha Mrajisi wa elimu Zanzibar, kuhakikisha ifikapo Desemba 31, mwaka huu kumpatia orodha ya majina ya shule zote za binafsi zinazodaiwa ada ya mwaka ili kufuata taratibu za kisheria.

Katika hatua nyingine, alitembelea Idara ya Kiswahili na lugha za kigeni kampasi ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), Vuga kuangalia maendeleo ya matengenezo ya vyoo pamoja na ukumbi wa mikutano na kuridhishwa na hatua inavyoendelea.

Pia, alitembelea Idara ya Mafunzo ya Ualimu, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Kitengo cha Ofisi ya Mrajisi wa Elimu Zanzibar na kitengo cha elimu mjumuisho Zanzibar.

Wakati huo huo, waziri huyo alitembelea ukarabati wa ujenzi wa maeneo mbalimbali ya Taasisi ya elimu na lugha za kigeni na kuridhishwa na maendeleo ya ukarabati huo.

Mkuu wa shule endelezi na utaalam, Dk. Haji Ali Haji, alisema hatua ya ukarabati inaendelea vizuri na wameamua kutengeneza choo cha watu wenye mahitaji maalum ambacho awali hakikuwapo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA KAZI

**Nafasi za kazi ya ualimu Diploma**
**- Kiswahili**
**-Science SST**
**- Kiingereza**
**Mawasiliano:**
**0783 334653**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI NA. 138/2020**

**MDAI: RAMADHAN ADAM LUMELEZI**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: FERUZI JUMA WA GEITA MJINI**

**AMRI:** Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani
mnamo tarehe 23/12/2020 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo IJUMAA tarehe 20 Novemba, 2020.

PRIMARY COURT MAGISTRATE
GEITA
HAKIMU

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LOICE MATAYO SHILLA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI CANTER **DYNA**
YENYE NAMBA YA USAJILI **T967 AKA**
CHASSES **NO BU600041484**
ENGINE **NO 1181563**
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
**ARU/ARU/RB/833388/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;362/2020**

**Ombi la GODFREY HENRY MLOKA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MARY HENRY KUNAMBI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/12/2020.

Tarehe 1/12/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

116026902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JONAS ESTOMIH NKYA** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 482 AYQ** aina yake NISSAN PATROL.Yenye chasis namba ***JNITESY61U0006582.***

Kwa yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi.**Rb namba MOR/MOR/RB/832484/2020.**

216027002

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**CHRISTOPHER B. NKINDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki iliyokuwa na namba ya usajili **MC 301 CAC** na chasis namba **MD2A21BY4JWC89256.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: IR/TR/RB/1678/2020**

116027202


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


## KUPOTEA KWA VYETI




116027302

**HALIDI A HAMIS** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **S0485-0225** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARY **MAJENGO** MWAKA **2010,**YEYOTE ATAKAYEKIOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**POLISI TAARIFA DAR/CEN/RB/834495/2020**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ABDULBASWAT SHWAIB SALEHE** anatangaza kupotelewa kwa result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.0671/0562** iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **UBUNGO ISLAMIC HIGH** mwaka **2020,** yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**Polisi taarifa DAR/MAG/RB/835098/2020**


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Watano wafa kwa mafuriko

**Bangkok,** THAILAND

NCHINI Thailand imeripotiwa vifo vya watu watano baada ya kukumbwa na mafuriko kutokana na mvua za masika katika majimbo saba kusini mwa nchi hiyo.

Mamlaka zilisema tukio hilo lilitokea jana, jimbo la Nakhon Si Thammarat.

Picha katika televisheni zilionyesha watu wakipiga kasia katika maji yaliyokatiza barabarani wakiwa kwenye boti.

Mafuriko hayo yalianza wiki iliyopita kwa mujibu wa wizara ya mambo ya ndani, yameathiri makazi 255,000 kwenye majimbo saba.

Eneo lililoathiriwa ni makao ya mashamba makubwa ya mpira nchini Thailand, kuliko maarufu kwa kilimo hicho mpira asili. **REUTERS**

## Tembo waongezeka wauzwa kwa mnada

**Windhoek,** NAMIBIA

WIZARA ya Mazingira, Misitu na Utalii, ya Namibia, imesema kwamba serikali inapanga kuuza ndovu 170, kutokana na hali mbaya ya kiangazi na idadi kubwa ya ndovu katika nchi hiyo ya kusini mwa Afrika.

Idadi ya ndovu imeongezeka kwa kasi nchini humo, kutoka 7,500 mwaka 1995 hadi kufikia 24,000 mwaka 2019.

Tangazo la kuuzwa kwa ndovu hao limetolewa na shirika la habari la serikali la New Era, ambalo limeripoti kuongezeka kwa visa vya ndovu kushambulia binadamu.

Pia kuna hatari ya kutoweka kutokana na uwindaji haramu pamoja na sababu za kimazingira. **VOA**

## Athari tabianchi zaiamsha UN

**New York,** MAREKANI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, ameikosoa jamii kwa kushindwa kupambana na ongezeko la joto duniani, akisema uongozi wa Marekani ni muhimu kushughulikia dharura ya mabadiliko ya tabianchi.

Katika hotuba yake aliyoitoa Chuo Kikuu cha Colombia, mjini New York, Guterres alionya kuwa hali ya sayari imevunjika na ubinadamu unasababisha vita vya asili.

Alisema viwango vya joto kali, ukame pamoja na bahari kufikia rekodi za juu za joto, zinasababishwa na utunzaji mbaya wa mazingira unaofanywa na mwanadamu.

Alitoa wito kudhibiti gesi chafu ya kaboni, mapambano ya janga la mabadiliko ya tabianchi kupewa kipaumbele katika karne ya 21. **DW**

# 'Bangi siyo dawa hatari'

**Washington,** MAREKANI

UMOJA wa Mataifa (UN), imepiga kura kuondoa bangi katika orodha ya kundi la dawa hatari zaidi, hatua ambayo inatambua mmea huo kwa manufaa yake kitiba.

Tume ya Umoja wa Mataifa ya kudhibiti dawa za kulevya, imeidhinisha pendekezo la Shirika la Afya Duniani (WHO), siku ya Jumatano, kuondoa bangi na utomvu wa bangi kutoka kwa kundi la dawa zenye kuhitaji kudhibitiwa kwa kipindi kirefu.

Dawa katika kundi hili linalojulikana kama 'Schedule IV' huchukuliwa sio tu za kulevya, lakini pia zinazofanya mtu kuwa mtegemezi.

**Pia huchukuliwa kuwa hatari na matumizi yake kimatibabu husemekana ni kwa kiwango kidogo sana.**

Pia huchukuliwa kuwa hatari na matumizi yake kimatibabu husemekana ni kwa kiwango kidogo sana.

"Hizi ni habari njema kwa mamilioni ya watu wanaotumia bangi kama dawa na pia kuna akisi ukuaji wa soko la bidhaa hiyo kwa misingi ya kimatibabu," kundi moja la utungaji wa sera za dawa limesema katika taarifa yake iliyotoa kwa wanahabari.

Kati ya nchi wanachama 53, ni 27 zilipiga kura kuunga mkono, huku 25 wakipinga kutambuliwa kwa bangi kama yenye manufaa, Ukraine ikijizuia kupiga kura.

Marekani na nchi za Ulaya ni miongoni mwa zile zilizopiga kura kuunga mkono, China, Misri, Nigeria, Pakistan na Urusi zikiwa miongoni mwa nchi zilizopinga utambuzi huo.

Hatua hiyo ya kihistoria inatarajiwa kufungua milango kwa mmea huo kutambulika kwa manufaa yake kama dawa na tiba na kuwa rahisi kwa nchi kufanya utafiti.

Bangi imekuwa katika orodha ya mimea inayodhibitiwa sana kwa miaka 59 na kuhamasisha watu ulimwenguni kutoitumia, isipokuwa kwa matumizi ya tiba. **BBC**



Wahamiaji wa Ethiopia wakiwasili katika uwanja wa ndege wa Ben Gurion karibu na Tel Aviv, Israel, jana. Mamia ya wahamiaji Waethiopia wamewasili Israeli, ikiwa ni hatua iliyochukuliwa na Isarel kutekeleza ahadi yake kuziunganisha tena familia zilizogawanyika kati ya nchi hizo mbili. **PICHA: AFP**

# Somalia: Kenya ina njama kutukosesha amani

**Mogadishu,** SOMALIA

WAZIRI wa habari wa Somali, Osman Abukar Dubbe, ameishutumu Kenya kwa njama ya kupanga kuikosesha Somalia amani, ikijitayarisha katika uchaguzi wa urais.

Kituo cha televisheni kinachomilikiwa na serikali kimeripoti.

"Tunaheshimu Kenya, tunafurahia ujirani wetu na maslahi ya pande zote mbili. Upande wetu, kanuni na misingi yetu tunaidumisha.

Hata hivyo, Kenya inaonekana kutojali hilo na badala yake inataka kutekeleza mambo yasiofaa na ni nchi ambayo dhamira yake ni kuchukua ardhi na sehemu ya majini ya Somali," alisema Dubbe.

Aliyasema hayo katika matangazo ya moja kwa moja kupitia televisheni ya taifa kwa njia ya kurasa ya Facebook.

Waziri Dubbe, ameishutumu Kenya kwa muingilio wa kisiasa na kuwa mwenyeji wa viongozi wa upinzani katika jiji la Nairobi.

Wanasiasa kutoka kusini mwa Somalia, eneo la Jubbaland, ni miongoni mwa wale ambao wamewahi kufanya mikutano mjini Nairobi, huku majadiliano ya uchaguzi wa Somalia mwaka 2020/2021 yakiendelea.

"Mogadishu haijawahi kuwa mwenyeji wa mwanasiasa yeyote wa upinzani kutoka Kenya, ambaye anataka kuharibu amani ya jirani zetu, lakini badala yake, Nairobi imekuwa ng'ombe ya mashambulizi yote dhidi ya Somalia.

Pia imekuwa eneo ambalo makubaliano yote yaliyofikiwa ndani ya Somalia yanakiuka.

Dubbe pia alisema kundi la kigaidi la al-Shabab liliteka maeneo kusini mwa Somalia, baada ya wanajeshi wa ulinzi wa Kenya ambao ni sehemu ya wanajeshi wa Umoja wa Afrika-Somalia (Amisom), kujiondoa kutoka kwa miji ya kimkakati eneo hilo.

Novemba 30, serikali ya Somalia ilimuita nyumbani balozi wake nchini Kenya na pia ikamtaka balozi wa Kenya nchini humo "kuondoka kwa ajili ya majadiliano". **BBC**

# ZIDANE APEWA MECHI NNE




**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amepewa mechi nne zitakazoamua hatima yake ndani ya klabu hiyo, kwa mujibu wa ESPN.

Hiyo ni kutokana na matokeo mabaya mfululizo kwenye Ligi Kuu Hispania na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Katika msimamo wa Kundi B wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, Madrid inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba, ambazo sawa na Shaktar Donetsk anayeshika nafasi ya tatu, Borrusia Monchegladbach anaongoza kundi hilo kwa pointi nane na Inter Milan anaburuza mkia kwa pointi tano.

Kwa mujibu wa mtandao wa Marca wa nchini Hispania, mtihani huo wa Zidane utaanza katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki hii dhidi ya Sevilla, kabla ya wiki ijayo kukutana na Monchegladbach katika mchezo wa mwisho wa Ligi ya Mabingwa utakaopigwa Uwanja wa Bernabeu.

Michezo mingine ni dhidi ya Atletico Madrid na Club yote ya La Liga.

# Pochettino awashiwa taa ya kijani Madrid

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, anapewa nafasi kubwa dhidi ya Raul kuchukua mikoba ya Zinedine Zidane pale Real Madrid, kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania.

Zidane aliiongoza Madrid kushinda mara tatu mfululizo taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati akiinoa timu hiyo kwa mara ya kwanza.

Msimu uliopita baada ya kurudi mara ya pili katika klabu hiyo aliyoichezea kwa mafanikio makubwa, alitwaa taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Lakini Los Blancos hao wamekuwa na wakati mgumu msimu huu kwa kuwa na matokeo mabaya.

Zidane yupo hatarini kupoteza kazi baada ya Jumanne kufungwa na Shakhtar Donetsk kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na hivyo kuweka rehani nafasi ya kufuzu hatua ya mtoano.

Los Blancos hao wamekumbana na vipigo mfululizo katika mechi tatu kati ya tano zilizopita na wamepitwa pointi saba na vinara wa LaLiga.

Gazeti la Mundo Deportivo la Alhamisi, liliripoti kwamba, kocha wa zamani wa Tottenham, Pochettino na kocha wa kikosi cha akiba cha Madrid, Raul wanawania nafasi yake.







# Solskjaer atoa neno kwa Fred

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anahisi Fred alikuwa na bahati ya kutotolewa nje kwa kadi nyekundu kwa faulo yake ya kwanza.

Fred alilimwa kadi nyekundu kipindi cha pili wakati United ikichezea kichapo cha mabao 3-1 kutoka kwa Paris Saint-Germain kwenye mechi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyofanyika Jumatano usiku.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alionyeshwa kadi ya njano katika kipindi cha kwanza kwa kumchezea faulo Leandro Paredes, kabla ya kupata ya pili iliyozaa nyekundu kwa kumkwatua Ander Herrera.

Solskjaer alilalamikia uamuzi wa kumtoa nje kiungo huyo, ingawa alikubali kwamba kipindi cha kwanza alikuwa na bahati ya kutotolewa nje.

"Tulizungumza nae kipindi cha pili. Nilifikiri kwamba alicheza vizuri sana," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Nafikiri kipindi cha kwanza alikuwa na bahati, kwa sababu ilionekana wazi kwamba angetolewa nje.

"Lakini alibahatika kutotolewa, lakini kwa uhakika kabisa kipindi cha pili kilikuwa kibaya zaidi kwake wakati tukipoteza."

HABARI MICHEZO

# Haaland nje ya dimba hadi mwakani

**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland atakuwa nje ya uwanja hadi Januari mwakani baada ya kuumia misuli na kocha wake, Lucien Favre, amebainisha straika huyo anahitaji kupumzika.

Fowadi huyo wa kimataifa wa Norway aliachwa kwenye mchezo wa Dortmund wa Jumatano dhidi ya Lazio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mabao ulimalizika kwa sare ya kufungana bao 1-1, baada ya kuumia kwenye mazoezi.

Amecheza mechi 14 kwa Dortmund katika mashindano yote msimu huu, akianza katika mechi 13 na kufunga mabao 17.

Hata hivyo, klabu hiyo itakuwa bila nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 kwa kipindi kilichobaki cha mwaka 2020 ambapo ni pigo kwa Favre.

"Hatacheza kabla ya mwanzo mwa Januari. Pengine amecheza sana," alisema Favre akiiambia Sky Germany.

"Mara ya kwanza hatukufikiri kwamba atakuwa kwenye hali mbaya namna ile. Lakini hawezi kucheza kwa sasa."

Dortmund imepitwa pointi nne na vinara wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich na itacheza na Eintracht Frankfurt, Stuttgart, Werder Bremen na Union Berlin kabla ya kumaliza mwaka.






# KOEMAN MATUMAINI KWA GRIEZMANN

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman anaamini, Antoine Griezmann, anaendelea kujiamini na kocha huyo wa Barcelona ana matumaini mshambuliaji huyo ataendelea kuwa kwenye kiwango cha juu zaidi.

Griezmann alifunga kwa mara ya tatu mfululizo kwa mara ya kwanza pale Barca wakati akiiweka mbele kwenye ushindi wa mabao 3-0 katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Ferencvaros, juzi Jumatano.

Martin Braithwaite alifunga la pili kabla ya Ousmane Dembele kufunga kwa penalti wakati kikosi hicho cha Barca kikiwa kimempumzisha nyota wake, Lionel Messi, kikiwa kinashinda mchezo wao wa tano wa makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2002-03.

Lakini kiwango cha Griezmann ndicho kilichomkuna zaidi Koeman na akamsifia fowadi huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

"Mara zote ni suala tu la kumwamini mchezaji. Kama nilivyosema mara nyingi, Antoine mara zote anajituma ili kujiimarisha na kuwa fiti kwa ajli ya mchezo," alisema.

# *Ronaldo afunga bao la 750*

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo aliwashukuru "wachezaji, makocha na wapinzani wake" baada ya nyota huyo wa Juventus kufunga bao la 750 katika maisha yake ya kandanda.

Ronaldo alifikisha idadi hiyo ya mabao baada ya kufunga dakika ya 57 wakati Juve ikiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Dynamo Kiev kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mechi ya Kundi G iliyochezwa juzi usiku.


Lilikuwa bao lake la 75 kwa Juve katika mashindano yote, baada ya kujiunga na timu hiyo akitokea Real Madrid ambako alifunga mabao 450.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 ambaye ni mshindi mara tano wa Ballon d'Or, alisema anawashukuru wachezaji wenzake kwa kumwezesha kufikisha idadi hiyo ya mabao.

"Mabao 750. Mabao 750 ya nyakati za furaha," aliandika.

"Nawashukuru wachezaji wote na makocha kwamba wamenisaidia kufikia hatua hii, nawashukuru sana na asante sana."

Ronaldo sasa ana nafasi ya kufikisha mabao 751 wakati atakapoichezea Juve dhidi ya Torino Jumamosi kwenye Ligi Kuu Italia.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR: NINATAKA KUCHEZA NA MESSI

## Mbrazil afunguka ndoto zake hizo baada ya kuisaidia PSG kutinga hatua ya mtoano...

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR aliibua maswali baada ya kuisaidia Paris Saint-Germain kupata ushindi dhidi ya Manchester United wakati aliposema anataka kucheza tena na Lionel Messi mwaka 2021.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil alifunga mara mbili kuisaidia PSG kupata ushindi wa mabao 3-1 kwenye dimba la Old Trafford, matokeo ambayo yaliwaweka wao imara zaidi ya kutinga hatua ya mtoano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar alijiunga na mabingwa hao wa Ligue 1 akitokea Barca kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222 mwaka 2017, huku akitajwa amekimbia 'kivuli' cha Messi pale Barcelona.

Miamba hao wa Katalunya walishinda mataji matatu msimu wa 2014-15 wakati safu yao ya ushambuliaji ikiongozwa na Neymar, Messi na Luis Suarez.

**Kuondoka kwa Neymar pale Barcelona kulitajwa kunaweza kumfanya nyota huyo wa zamani wa Santos kushinda tuzo ya Ballon d'Or.**

Neymar mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi tena nchini Hispania, lakini aliweka wazi kwamba atabakia jijini Paris angalau hadi mwishoni mwa msimu wa 2020-21.

Messi alishindwa katika mpango wake wa kutaka kuondoka Barca katika dirisha lililopita, lakini mkataba wake unamalizika Juni mwakani, na bado haijulikani kama atabakia au ataondoka.

Kwa upande wake Neymar, kitu pekee anachokitaka kwa sasa ni kucheza tena na mchezaji mwenzake huyo, akiambia ESPN kwamba: "Nataka sana kucheza tena na Messi.

"Nataka kucheza naye. Nitamwambia cheza kwenye nafasi yangu kama anataka!"Mwakani, tunatakiwa kucheza pamoja, kwa uhakika kabisa."

Mabao mawili ya Neymar dhidi ya United yalimfanya kufikisha mabao 38 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

## ZISIKUPITE

### INTER KUMUUZA SKRINIAR

KLABU ya Inter Milan inajiandaa kumuuza mlinzi wake, Mslovakia Milan Skriniar, 25, kwa Tottenham kwa ada ya pauni milioni 45 ifikapo mwezi ujao. ***(Sun)***

### SCHUURS: SIONDOKI AJAX

BEKI wa kati wa Uholanzi, Perr Schuurs, 21, aliyehusishwa na taarifa za kuhamia Liverpool, anasisitiza kuwa hayuko tayari kuondoka Ajax. ***(Mirror)***

### POCHETTINO AKARIBIA

KOCHA wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino, anaongoza mbele ya kocha wa kikosi cha akiba cha Real Madrid, Raul, kama mwalimu anayepewa nafasi kubwa ya kuchukua mikoba ya Zinedine Zidane, iwapo Real wataamua kumfuta kazi Mfaransa huyo. ***(Marca)***

### MOYES, WEST WATETA

KLABU ya West Ham ipo katika mazungumzo na kocha David Moyes kuhusu kuongezwa kwa mkataba wake, ambao unamalizika msimu huu. ***(Sky Sports)***

### ZIDANE AMKATAA HAZARD

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane amepoteza imani na wachezaji wake kadhaa ikiwa ni pamoja na winga wa zamani wa Chelsea, Eden Hazard, 29, ambaye ni mchezaji wa kimataifa kutoka Ubelgiji. ***(Sport)***

### TERRY AMTAJA COLE

KOCHA Msaidizi wa Aston Villa, John Terry atamtafuta mchezaji mwenzake wa zamani wa Chelsea, Ashley Cole kushikilia nafasi ya kazi katika utawala wake wa timu kama atateuliwa kuchukua kazi ya kudumu ya Kocha, Phillip Cocu. ***(Mirror)***

### DELE NJIA PANDA

KOCHA wa Tottenham, Jose Mourinho, anasema ni jukumu lake kuamua iwapo klabu hiyo itamuuza kiungo wa kati wa England, Dele Alli, 24, wakati wa dirisha la usajili la Januari au la. ***(Telegraph - subscription required)***

### YAMTAKA WILLIAMS

KLABU ya Newcastle imekuwa ikimfuatilia kwa karibu mchezaji wa Manchester United, Brandon Williams, 20, anayecheza nafasi ya mlinzi wa kushoto katika kikosi cha vijana walio chini ya umri wa miaka 21 cha England, anaweza kupatikana kwa mkataba wa mkopo ifikapo Januari. ***(Newcastle Chronicle)***

### ARTETA AJIPANGA JANUARI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, anasema yeye pamoja na Mkurugenzi wa Ufundi, Edu, wanafanya mpango kwa ajili ya kipindi cha dirisha la uhamisho la Januari na kile kinachoweza kuwa soko 'lisilotarajiwa'. ***(London Evening Standard)***

### RASHICA HAUZWI- BREMEN

KLABU ya Werder Bremen imeachana na mpango wa kumuuza kiungo wake wa kati, Milot Rashica, Januari licha ya taarifa kwamba, Aston Villa wanaweza kurejea nia yao kwa kijana huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Birmingham Mail)***

## Julio afunguka siri kichapo U-20

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupokea kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Uganda, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), Jamhuri Kihwelo 'Julio', ametaja sababu iliyopelekea kupata matokeo hayo mabaya ni wachezaji wake kupoteza ari ya kupambana.

Julio alisema baada ya Ngorongoro Heroes kukata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2021), wachezaji wake hawakucheza katika kiwango chao kilichozoeleka.

Kocha huyo alisema wachezaji wake hawakuwa sawa kisaikolojia kwa sababu ya kufahamu tayari wameshafuzu AFCON, hali iliyosababisha washindwe kujituma kama walivyofanya katika mechi zilizopita.

"Wachezaji walikosa ari ya kupambana, kutokana na kuona tayari wamefuzu, lakini wenzetu walikuja kulipiza kisasi cha mwaka jana tulichowafanyia kule kwao, tumefanya makosa mengi ambayo tumeadhibiwa," alisema Julio.

Aliongeza ataendelea kukiimarisha kikosi chake ili kiwe imara kabla ya kwenda kwenye fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Mauritania.

## KVZ yawatangazia hatari Wasudani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa KVZ, Sheha Khamis, amesema anaamini kikosi chake kitafanya vizuri na kusonga mbele katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika CAF licha ya kuanza vibaya kampeni ya kuwania taji hilo.

KVZ inatarajia kuwakaribisha El Amal kutoka Sudan utakaochezwa kesho kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan.

Sheha alisema kikosi chake kinaendelea vyema na maandalizi ya mchezo huo na wamejiandaa kuonyesha kiwango bora kwenye mechi hiyo ya marudiano.

Alisema malengo yao ni kuona wanasonga mbele na wanaamini inawezekana endapo wachezaji watafanya kile alichowaelekeza mazoezini.

"Tumejiandaa kupata ushindi utakaotufanya tusonge mbele katika michuano hii, lengo letu ni kuhakikisha tunafikia hatua ya makundi lakini ili tufikie huko ni lazima wachezaji wawe na jitihada na hamu ya kucheza mpira, hatutaki kuwa washiriki, tutapambana ili lengo letu litimie," alisema Sheha.

Kocha huyo amewaomba Wazanzibar na mashabiki wote wa soka visiwania hapa kuungana pamoja ili kuipa nguvu KVZ ambayo inawakilisha nchi katika mashindano hayo ya kimataifa.

Kikosi cha El Amal ambacho katika mechi ya kwanza kilipata ushindi wa bao 1-0, kinatarajiwa kuwasili Zanzibar leo mchana.

# MWINYI AVIFUNDA VYAMA, MLANDEGE 'YAPIGWA' TAFU

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameitaka Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuhakikisha vyama vyote vya michezo vinaandaa taratibu zitakazowavutia wadhamini, zaidi ya Sh. milioni 78 zimechangwa ili kuisaidia Mlandege inayoshiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Dk. Mwinyi alisema hayo Ikulu Visiwani hapa katika hafla ya makabidhiano ya fedha zilizotolewa na wafanyabiashara watano wa Zanzibar kwa ajili ya kufanikisha ushiriki wa timu ya Mlandege ambayo inajiandaa na mechi ya marudiano dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia.**

Alisema maendeleo ya michezo hapa nchini yatafikiwa endapo udhamini wa uhakika na wenye kunufaisha pande zote mbili utakuwapo.

Kiongozi huyo aliwataka wafanyabiashara kote nchini kujitokeza kusaidia maendeleo ya michezo, ikiwamo soka ili kurejesha hadhi ya mchezo huo iliyopotea na kuongeza taifa lina wajibu wa kuhakikisha michezo inaimarika.

Aliwakumbusha viongozi wa vyama vya michezo kukaa na wadau ili kuimarisha ushirikiano na uhusiano kwa ajili ya kufikia maendelea.

Aliwashukuru pia wafanyabiashara hao kutoka kampuni mbalimbali kwa kutoa fedha za kuisaidia Mlandege kusafiri kuelekea Tunisia katika mchezo huo.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Mwita Maulid aliahidi kukaa na wadau ili kuimarisha maendeleo ya michezo pamoja na kuanza mapema maandalizi ya mashindano yajayo ya Kombe la Mapinduzi.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Omar Hassan Omar 'King' aliishukuru serikali kwa wito wake wa kuitaka wizara hiyo kuwakutanisha na wadau wa michezo ili kufanikisha safari ya kikosi cha Mlendege.

King alisema baada ya kubaini kiwango cha michezo kimeshuka Visiwani hapa, kwa kushirikisha na Chama cha Mapinduzi, watahakikisha wanaboresha miundombinu kuanzia ngazi ya wilaya.

Alisema pia bado katiba yao ina upungufu na hivyo wanahitaji kuifanyika marekebisho ili iendane na vyama vingine ambavyo ni wanachama wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na Fifa.

Nao, wafanyabiashara waliofadhili fedha hizo, walisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwashirikisha wadau wa michezo katika kila hatua ili kufanikisha maendeleo ya michezo nchini, ikiwemo soka.

Akitoa shukrani, Mkurugenzi wa Mlandege, Ali Khatibu Dai aliwashukuru wafanyabiashara hao kwa kujitolea kufanikisha safari ya timu yao ambayo inakwenda kupeperusha bendera ya Zanzibar.

Alisema kikosi cha Mlandege kitaondoka Zanzibar leo na kuelekea Tunisia kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidi ya SC Sfaxien utakaochezwa kesho mjini Tunis.



Golikipa wa timu ya KMC, Juma Kaseja, akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mgosi afurahia pointi nne ugenini

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema anawapongeza wachezaji wake kupambana kupata pointi nne ugenini na sasa wamerejea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kuonyesha makali yao katika mechi zinazofuata za ligi hiyo.

Simba walianzia ugenini kwa kushinda mabao 4-0 dhidi ya Mapinduzi Queens, mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa Sabasaba Iringa na juzi ililazimishwa suluhu na wenyeji, Ruvuma Queens, Uwanja wa Majimaji Songea.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mgosi alisema haikuwa kazi rahisi kupata pointi nne ugenini na anawashukuru wachezaji wake kupambana kulinda heshima ya kikosi chao.

Mgosi alisema wamerejea nyumbani kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao dhidi ya JKT Queens ambao wanatarajia pia utakuwa na ushindani kutokana na uimara wa kikosi cha wapinzani wao.

"Kuna makosa tulifanya katika mechi yetu dhidi ya Ruvuma Queens, tunayafanyia kazi kuelekea mchezo unaokuja, lakini pia tunawafahamu JKT Queens, hivyo tutaingia uwanjani tukiwaheshimu wapinzani wetu, kwa sababu malengo yetu bado yapo pale pale ni kutetea ubingwa wetu," alisema Mgosi.

Simba Queens itawakaribisha JKT Queens katika mchezo wa raundi ya tatu utakaochezwa Desemba 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena jijini.

# Michezo

Ijumaa Desemba 4, 2020

Nipashe





Neymar: Ninataka kucheza na Messi UKURASA 22

# Ntibazonkiza: Tukutane uwanjani

## Kiungo mpya Yanga afunguka amekuja kufanya kazi na...

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI mpya wa Yanga, Said Ntibazonkiza, amesema hatawaangusha viongozi na mashabiki wa klabu hiyo na kuahidi atafanya kile ambacho wanakitarajia kutoka kwake ili kusaidia timu hiyo kufikia malengo yake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

**Ntibazonkiza alitua nchini juzi usiku na kupata mapokezi kutoka kwa mashabiki wa Yanga ambayo wamefurahia ujio wake.**

Akizungumza na gazeti hili, Ntibanzokiza alisema anatarajia kutumia uzoefu wake kuisaidia Yanga kupata matokeo mazuri ambayo yanasubiriwa na mashabiki na wanachama wao.

"Nimefurahi kuona mapokezi haya, hii ni ishara kubwa kwamba nina deni kwao, kweli nikiwa Burundi nilifanikiwa kuangalia mechi za Yanga, ni timu nzuri ukizingatia bado inaongoza ligi, jukumu langu ni kwenda kufanya kazi na kuongeza uzoefu wangu ndani ya kikosi."

"Mchezaji yoyote anapokwenda timu mpya lazima akutane na ushindani, hasa suala la namba, kikubwa nimekuja kufanya kazi, sina maneno mengi zaidi kuwaambia zaidi ya kuwataka tukutane uwanjani," alisema Ntibazonkiza.

Aliongeza kwa kushirikiana na wachezaji wenzake, kwao kila mechi itakuwa sawa na fainali kwa sababu wanahitaji kuendelea kukaa kileleni kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Hatutadharau mechi yoyote, timu zote zinazoshiriki ligi ni sawa, kupitia kocha wetu, ninaamini kocha wetu atazidi kutuimarisha ili kucheza katika kiwango cha juu, hatutakata tamaa," mshambuliaji huyo alisema.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya GSM, Hersi Said na Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz, walikuwa ni baadhi ya viongozi waliofika kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere kumpokea nyota huyo.

Ntibanzonkiza alisaini mkataba wa miaka miwili na Yanga na usajili wake utaanza rasmi baada ya kufunguliwa dirisha dogo ifikapo Desemba 15, mwaka huu.

Yanga imeendela kujiimarisha ili kuhakikisha msimu huu inawavua watani zao, Simba ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wanaushikilia kwa misimu mitatu mfululizo. Kikosi cha Yanga kinaendelea na mazoezi chini ya Kocha Mkuu, Cedric Kaze kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Uhuru.

Simba ambao wanashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, tayari wameshamsajili kiungo mkabaji, Taddeo Lwanga kutoka Uganda.




Nahodha wa Simba, John Bocco (kushoto), akiwania mpira dhidi ya kiungo, Clatous Chama, katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya marudiano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Plateau United kutoka Nigeria, itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# Plateau United watua na neno

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Plateau United kinatarajiwa kuwasili nchini leo tayari kuwavaa wenyeji wao, Simba katika mchezo wa marudiano wa mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliliambia gazeti hili jana maandalizi na taratibu zote za kiitifaki kuelekea mchezo huo zimekamilika.

"Kutakuwa na taratibu zote zinazohusiana na COVID 19, naomba hili tulizingatie wote, tutaweka vitakasa mikono kwenye mageti yote, ni muhimu tuvae barakoa, wenzetu bado hili gonjwa wanalo, hapa wakifika wanatushangaa," Manara alisema.

Manara alisema anaamini mchezo huo wa marudiano utakuwa wenye burudani na ushindani kutoka pande zote mbili baada ya kufahamiana katika mchezo wa kwanza uliochezwa wiki iliyopita kwenye Mji wa Jos nchini Nigeria.

Simba itawakaribisha Wanigeria hao wakiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa bao 1-0, walilofunga kwenye mchezo wa kwanza walipokuwa ugenini, shukrani kwa Mzambia Clatous Chama ambaye alipachika wavuni goli hilo.

# Lwandamina rasmi Azam

**Na Saada Akida**

MZAMBIA George Lwandamina amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuiongoza Azam FC ambayo hivi karibuni ilitangaza kuachana na aliyekuwa kocha wake mkuu, Aristica Cioaba.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema tayari wameshamwandalia Lwandamina usafiri wa kuungana na kikosi cha timu yake kwa ajili ya kuanza rasmi majukumu yake.

"Nimefurahi kuja kwa mara nyingine Tanzania, nilikuwapo nikaondoka na sasa nimerudi tena kukinoa kikosi cha Azam, imani yangu kuwa pamoja katika mafanikio ambayo yanatarajiwa na uongozi pamoja na mashabiki wa timu hii," alisema Lwandamina.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042